SportPesa
TZS. 595,659,980
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Mganga** afungwa jela miaka 30 kumbaka mke wa rafiki yake

UKURASA 3



Tufikirieni saa za baa penye kodi, ajira zaidi

BUFE
IJUMAA OKTOBA 22, 2021 Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Ngozi ya mnyama; utajiri ambao wengi hawajazinduka kutambua thamani yake

Ukurasa 12

MATUNDA YA WORLD VISION...

**Mwenye ulemavu, fundi tangu 1978 aunganisha na kilimo kuona mageuzi**

• Kutoka kutegemea, hadi kutegemewa

Na Renatha Msungu, CHEMBA

NI kama hadithi, lakini uhalisia ndio huo ni mwanamke mwenye umri wa miaka 60, mwenye ulemavu wa miguu anayejishughulisha na kilimo cha kisasa, huku cherehani anayotumia kushona katika makazi yake, eneo la Kwamtoro, wilayani Chemba, Dodoma.

Grace Andrea ni mama wa wajukuu wawili wa kike walioko shule ya sekondari, akiwatunza kupitia kazi hiyo ya kilimo cha kisasa, baada ya kupata mafunzo na mbegu bora kutoka Shirika la World Vision.

Leo yamemuwezesha hivi sasa kupata mazao mengi katika eneo la ekari chache anazolipa tofauti na ilivyokuwa mwanzo, alikuwa akipata mazao kidogo kwa kutotumia Kilimo cha kisasa.

World Vision, shirika lililojikita katika kusaidia watu wa hali ya chini kupitia miradi mbalimbali, inayoendesha pia wanamradi wa boresha afya ...

... imbali hapa nchini, ikiwamo Dodoma, ikiendesha mafunzo ya kila mara kwa jamii, kuhakikisha wanainuka kiuchumi, ikiwamo kilimo na biashara, hasa vijijini.

Grace Andrea ni mwenye ulemavu, mnufaika anayesema matokeo chanya ya mafunzo ya kilimo yatolewayo, ndio imezaa matunda hayo.

Anafafanua kuwa, kupitia kilimo ambacho anafanya, sasa anasomesha wajukuu zake na kuendesha maisha ya familia inayomtegemea kimaisha.

Grace anaiwekea shukrani muwezeshaji wake, asasi ya World Vision, ambayo imekuwa ikimtembelea kila anapoiita kujua maendeleo yake katika kilimo na ushonaji anaoufanya, kuhakikisha anasonga mbele katika maisha.

Anasema, aliamua kufanya hivyo, ili kuepuka kukimbiwa na jamii kutokana na kuamini mtu akiwa mlemavu basi hawezi kufanya kazi ...

... sasa anasomesha wajukuu na kulisha familia yake.

KUTOKA WORLD VISION

Joseph Kilimba, ni msimamizi wa miradi inayowainua kinamama kiuchumi, anasema shirika hilo limekuwa likiwapatia mafunzo ya kilimo, ikiwamo kuwapa mbegu bora kinamama na jamii kwa ujumla, kuwapa tija.

Hivi sasa kuna kinamama wengi ambao wameunda vikundi vya vikoba kupitia kilimo wakiwa na mafamikio na World Vision, wamekuwa wakiwapita kila mara kuviangalia.

Anasema, wanafurahi kuona kinamama hao hawabaki nyuma, japo wapo ambao wamekuwa wazito kuhudhuria mafunzo ambayo ni muhimu sana kwao, katika kuendeleza familia zao.

Kilimba anasema, pia wanawafundisha kutengeneza lishe bora, ambacho wanatengeneza na kuwauzia wengine, ili kuhakikisha afya za watoto wao zinakuwa bora.

Anafafanua kuwa, lengo lao ni kuona kinamama wanapata mafunzo kutoka World Vision na kupiga hatua, wakawa mfano wa kuigwa kimaisha, huku wakiwa na kipato cha kuwainua kiuchumi ...

UKURASA 11


Ijumaa Oktoba 22, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580741

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# Rufani hukumu ya Ole Sabaya

**MAWAKILI** wake waweka kusudio, Vodacom yatoa sababu kutoa mawasiliano yake mahakamani... *Endelea ukurasa 2*

UKURASA WA 4

## MUME NA MKE WAUAWA WAKIWA WAMELALA USIKU

WATU wawili, mke na mume, Anes Haule (45) na Menluph Ngailo (45) wameuawa kwa kukatwa katwa mapanga wakiwa wamelala nyumbani kwao katika kijiji cha Itacha, Ludewa mkoani Njombe...

UKURASA WA 4



## HAKIMU AKWAMISHA HUKUMU KINA AVEVA

ALIYEKUWA Rais wa Klabu ya Simba, Evans Aveva, na Makamu wake, Godfrey Nyange, maarufu Kaburu, jana walitumia muda mwingi kukaa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu...

UKURASA WA 2



## LHRC YAMTUNUKU MWANDISHI NIPASHE

MKURUGENZI Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, amevipongeza vyombo vya habari vya IPP kwa kuwa mfano katika kuwapa nafasi waandishi wake kufanya habari...

UKURASA WA 4

## SERENGETI YASHINDA TUZO HIFADHI BORA

HIFADHI ya Taifa Serengeti imeshinda tuzo ya hifadhi bora inayoongoza Afrika kwa mwaka 2021, iliyotolewa na World Travel Awards (WTA). Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya...

# MACHINGA WAPEWA SAA 18 KUHAMA

UKURASA 3




Gari la Jiji la Mwanza, likiwa na askari mgambo likipita katika mitaa mbalimbali jijini jana, kwa ajili ya kuondoa vibanda vya wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga wanaofanya shughuli zao kwenye maeneo yasiyoruhusiwa na kushindwa kuviondoa wenyewe. **PICHA: RICHARD MAKORE**

# PAC yabaini dosari nne Deni la Taifa

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA SC YAITANGAZIA GALAXY 'IT'S NOT OVER' UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga (kushoto), akikabidhi cheti cha pongezi kwa Mhariri wa Habari wa gazeti la Nipashe, Sanula Athanas, katika chumba cha habari cha The Guardian Ltd, Mikocheni, Dar es Salaam jana, baada ya kushinda Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2020, kipengele cha Habari za Haki za Binadamu na Utawala Bora. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Rufani hukumu ya Sabaya

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

ALIYEKUWA Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, na wenzake wamewasilisha taarifa ya kusudio la kukata rufani Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, kupinga hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha dhidi yao.

Oktoba 15, mwaka huu, mahakama hiyo iliwahukumu kifungo cha miaka 30 Sabaya na wenzake watatu baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la unyang'anyi wa kutumia silaha.

Wakili Moses Mahuna alinukuliwa akidai kuwa baada ya kuwasilisha taarifa ya kusudio hilo la rufani jana, taratibu zingine zinaendelea.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Arusha, Odira Amworo, baada ya kuridhika kuwa upande wa mashtaka umethibitisha mashtaka dhidi ya Sabaya na wenzake.

Kabla ya kushtakiwa, uteuzi wa Ole Sabaya katika nafasi ya Mkuu wa Wilaya ya Hai ulitenguliwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Ole Sabaya pia anakabiliwa na kesi nyingine ya uhujumu uchumi inayoendelea kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha, ikiwajumuisha washtakiwa wengine sita.

# PAC yabaini dosari nne Deni la Taifa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (PAC) imechambua Deni la Taifa na kubaini kuwa ni himilivu.

Hata hivyo, kamati hiyo imebaini dosari nne kwenye deni hilo, ikiwamo baadhi ya taasisi kukopa takribani Sh. bilioni 896 bila kupata kibali cha Waziri wa Fedha.

Akizungumza na Nipashe mara baada ya mahojiano kuhusu hoja za ukaguzi za CAG kwa mwaka 2019/20, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Japhet Hasunga, alisema kamati imechambua deni hilo na mambo mengi imeridhika nayo.

Alisema PAC imeangalia uhimilivu wa deni na vigezo vinavyotumika ambapo huangalia thamani ya deni kwa kulinganisha na uchumi wa nchi.

"Tumeangalia viwango vinavyokubalika ambapo imeonekana deni letu ni himilivu na halina shida, lakini changamoto iliyopo nchi imeingia katika kipato cha kati, kwa hiyo ina maana hata vigezo vya mkopo vinabadilika. Baada ya muda vitabadilika ili tujue vigezo vyetu sasa ni vipi," alisema.

Hasunga alisema katika uchambuzi huo kamati imebaini kutokuwapo kwa mfumo mzuri wa utunzaji kumbukumbu ambapo katika mfumo uliopo, baadhi ya madeni hayaonekani au kumbukumbu zake hazipo sawa.

"Tumeagiza serikali waje na mfumo madhubuti utakaosaidia katika utunzaji wa kumbukumbu na kuweza kujua mkopeshaji ni nani, masharti ya ukopeshaji yakoje na taratibu za ulipaji zikoje? Kwa hiyo, ile mikataba yote na taratibu zote ziwapo kwenye huo mfumo," alisema.

Aliongeza kuwa kuna madeni ya baadhi ya taasisi Sh. bilioni 896 ambayo taasisi zimekopa bila kupata kibali cha Hazina na Waziri wa Fedha.

"Madeni hayo pamoja na kwamba yalikuwa ni muhimu, lakini tunadhani kwamba taasisi kwa sasa inapotaka kukopa lazima ihakikishe inapata kibali cha Hazina na fedha zinatolewa kwa mujibu wa taratibu.

"Ni kwa sababu haya madeni ni mengi na taasisi ni nyingi zilizokuwa zinahusika katika kipindi hicho kwa ajili ya kuigharamia miradi mbalimbali ya maendeleo," alisema.

Hasunga alisema suala lingine lililoonekana ni kutokuwa na usimamizi mzuri wa deni la taifa na kutaka kuwapo na usimamizi mzuri na takwimu zote na kila kitu kikae kwenye idara moja.

"Kwa sasa serikali imepitisha muundo mpya wa usimamizi wa Deni la Taifa na mambo mengine ambapo wanataka hilo lijitegemee, hivyo kuanzia Julai Mosi, 2022 wanatarajia sasa Deni la Taifa litahama kutoka Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali fungu 22 na kwenda fungu 21 Hazina," alisema.

Makamu Mwenyekiti huyo alisema wanaamini kumbukumbu na taarifa zake zote za Deni la Taifa zitashughulikiwa na Hazina.

"Tunataka kuhakikisha kumbukumbu zinatimilika na zinakuwa kamilifu na huo uhamisho usiathiri wala kupoteza kumbukumbu ya aina yoyote kitu ambacho kitaleta madhara kwa taifa," alisema.

Hasunga alisema kamati imebaini baadhi ya wakopaji hawaheshimu taratibu za ulipaji wa madeni hayo na kuisababishia serikali kuwa na madeni makubwa.

"Kwa mfano unakuta halmashauri zimekopa au mashirika yamekopa ama nje au ndani lakini inapofika kipindi cha kulipa hawalipi kama inavyotakiwa na kuisababishia serikali madeni makubwa bila sababu za msingi," alisema.

Kamati hiyo iliagiza kuwa kila anayekopa azingatie sheria ya mikopo kama inavyowataka kuwa kila anayekopa ahakikishe analipa.

# LHRC yamtunuku mwandishi Nipashe

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, amevipongeza vyombo vya habari vya IPP kwa kuwa mfano katika kuwapa nafasi waandishi wake kufanya habari za uchunguzi zikiwamo zinazohusu haki za binadamu na utawala bora.

Anna aliyasema hayo jana alipozuru makao makuu ya Kampuni ya The Guardian yaliyopo Mikocheni mkoani Dar es Salaam kwa ajili ya kumpongeza Mhariri wa Habari wa Nipashe, Sanula Athanas, kwa kuwa mshindi kwa miaka miwili mfululizo wa Tuzo ya Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) kwenye kipengele cha Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Tuzo hizo za EJAT zimekuwa zikiandaliwa kila mwaka na Baraza la Habari Tanzania (MCT).

"Tumekuja kumpongeza Sanula ambaye ni mwandishi wa Nipashe, amepata tuzo za EJAT mfululizo kwa miaka miwili katika kipengele hiki cha haki za binadamu, kama watetezi wa haki za binadamu tunapenda watu waandike habari za haki za binadamu.

"Tunatoa zawadi hii ili kumtia moyo na waandishi wengine wawe wanafanya habari za uchunguzi kwenye muktadha wa haki za binadamu, tunapongeza gazeti la Nipashe, kampuni kwa ujumla kwa kutoa nafasi kwa waandishi wake kufanya habari za uchunguzi, hiki ni kituo cha mfano," Anna alisifu.

Alisema waandishi wa habari wa IPP wamekuwa wakiandika habari za haki za binadamu na kutoa wito kwao kuzipeleka kwenye mashindano ili kuzishindanisha kwa lengo la kutambulika kitaifa na kimataifa.

"Tupo tayari kutoa ushirikiano muda wowote kwa sababu hatuwezi kufika kila mahali nchini, lakini kupitia waandishi wa habari tunaweza, tunawategemea sana katika kufikisha habari za haki za binadamu," alisema.

Sanula aliushukuru uongozi wa gazeti la Nipashe na kampuni ya The Guardian kwa ujumla kwa kumpa nafasi ya kufanya kazi hizo.

"Siri ya mafanikio ni kujituma na kushirikiana na wadau kujua nini hasa kinaikwaza jamii, nimeshinda tuzo ya mwandishi bora wa haki za binadamu na utawala bora kwa mwaka 2019 na 2020 kutokana na ushirikiano niliopewa na wadau na uongozi wa kampuni.

"Mwaka 2019 nilikuwa mshindi katika kipengele hiki kutokana na ripoti yangu ya namna rushwa ya ngono inavyofanyika vyuo vikuu ikihusisha mhadhiri kwa mwanafunzi, mwanafunzi kwa mwanafunzi, mhadhiri kwa mhadhiri na ofisa utawala chuoni na mfanyakazi wa ngazi ya chini.

"Kwa mwaka 2020 niliandika kuhusu kijiji kilichoko Shinyanga Vijijini ambacho tangu kianzishwe mwaka 1974, kwenye Operesheni Vijiji ya Mwalimu Nyerere, hakijawahi kuwa na zahanati na mpango wa MAM wa mwaka 2007 tulioanza kutekeleza mwaka 2008, unataka kila kijiji nchini kiwe na zahanati," Sanula alifafanua.

Katika hafla hiyo, LHRC walimtunuku Sanula cheti cha pongezi kwa kuwa mshindi

**HABARI KITAIFA**

# Machinga wapewa saa 18 kuhama

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Robert Gabriel, ametoa saa 18 kwa wafanyabiashara wadogo, maarufu kama machinga, walioko eneo la Makoroboi, jijini Mwanza, kuondoka na kwenda katika maeneo rasmi waliyotengewa.

Mhandisi Gabriel alitoa agizo hilo jana alipotembelea eneo hilo kwa ajili ya kujiridhisha kama wafanyabiashara hao wametekeleza agizo la kuondoka baada ya muda wa makubaliano kuwapo hapo kupita.

Hali ilikuwa tofauti baada ya kukuta shughuli za biashara zikiendelea na hakuna anayefunga au kuwapo kwa harakati zinazofanyika za kuvunja vibanda vyao.

Alisema anaupongeza uongozi wa machinga kwa mapenzi yao kusema wataonyesha mfano kuondoka hapo na wengine wote waliozuia ofisi nyuma, mbele na kuzuia shughuli mbalimbali kufanyika mara baada ya nafasi kupatikana .

Pia alisema baada ya makubaliano hayo, waliomba wapate nafasi nzuri zaidi ya kufungasha vitu vyao na walipatiwa huku kuanzia wiki iliyopita hadi jana, walikuwa wanakumbushwa kuondoka katika maeneo ambayo si rasmi lakini kiuhalisia bado hawajaanza kufungasha wala kuondoka.

"Nipo hapa na timu nzima hakuna kinachoendelea na kinachofanyika na hamna mtu anayefunga hapa. Tulichokubaliana ni kinyume, bado watu wapo, hivyo mwisho leo (jana) kama tulivyokubaliana," aliyasema hayo wakati akizungumza na uongozi wa machinga ambao ni wamiliki wa vibanda hivyo kwa njia ya simu.

Mhandisi Gabriel alisema walikubaliana kuwa wataachia eneo hilo na kuondoka na kwamba waliomba wapewe muda hadi jana kwa ajili ya kufungasha. Aliwapigia viongozi wao wakasema wamechelewa kuanza kufanya hivyo lakini kiujumla vibanda vyote vinaondoka ili viachie njia kupisha maduka waliyoyaziba .

"Hapa mbele kuna vibanda vya machinga lakini huku nyuma kuna jengo lenye maduka, ofisi na wao wana kazi zao za kufanya. Tayari hivi ni vizuizi kwa hiyo lengo kubwa ni watu waondoke japokuwa wamesema wako tayari kulipia TRA.

"Kama uko tayari kulipia kuna kanuni lazima uwe na ofisi. Sasa hii si hadhi ya ofisi kwa hiyo tumewatambua walio tayari kulipa kodi lakini inabidi watuachie maeneo yote," alisema.

Mkuu huyo wa mkoa alisema kazi ya kusafisha maeneo yote mkoani hapa inaanza na itakuwa endelevu. Alisema mitaro yote itasafishwa, njia kupitika na hiyo inafanyika ili kuweka mazingira kuwa safi na yenye kuvutia.

"Wote waliopewa tiketi kwa ajili ya kwenda kwenye maeneo waliyopangiwa nawahimiza waendelee kuyashika maeneo yao. Kesho (leo) hapa kazi itakuwa kubwa, hakutaingilika wala kutoka. Nitoe wito kwa wananchi kuendelea kutekeleza hili jambo ambalo limeanza na sasa liko hatua nzuri za mwisho, hivyo waimalizie hiyo kazi kubwa ambayo ameshaianza," alisema.

**"Nipo hapa na timu nzima hakuna kinachoendelea na kinachofanyika na hamna mtu anayefunga hapa. Tulichokubaliana ni kinyume, bado watu wapo, hivyo mwisho leo (jana) kama tulivyokubaliana," aliyasema hayo wakati akizungumza na uongozi wa machinga ambao ni wamiliki wa vibanda hivyo kwa njia ya simu.**


## TANGAZO LA MNADA/NOTISI

MALAPA AUCTION MART CO.LTD. KWA NIABA YA CRDB BANK PLC TUNATOA NOTISI YA SIKU 14, TANGAZO NA TAARIFA KWA WAMILIKI WA DHAMANA ZIFUATAZO, WAWE WAMELIPA MADEN! YAO YOTE YA CRDB PAMOJA NA GHARAMA ZA DALAL!, YINGINEVYO TUTAUZA DHAMANA ZAO KWA MNADA WA HADHARA lIl KUFIDIA MADENI YAO YOTE.

| NO | MMILIKIIMDHAMINI | DHAMANA | USAJILI | MAHALI ILIPO | TAREHE/MUDA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | HASSAN KIMOLO CHEPA | NYUMBA | TITTLE 27940 L0.438969 | PLOT NO 33 BLOCKV KONDOA | 6 NOV. 2021 SAA 5 ASUBUHI |
| 2 | AHMEDI MUSSA KIDUKA | NYUMBA | TITTLE 14214 LO.161164 | PLOT NO 91 BLOCK BB KONDOA | 6 NOV. 2021 SAA8 MCHANA |
| 3 | PRIMOS M.TARIMO | NYUMBA | HATI VA MAUZIANO | MURIET/ KWAMROMBO ARUSHA | 8 NOV. 2021 SAA 5 ASUBUHI |
| 4 | WILFRED HIZA KUAZ | NYUMBA | TITTLE 45953 LO.331678 | PLOT NO 21 BLOCK E LONGIDO-ARUSHA | 9 NOV. 2021 SAA6 MCHANA |
| 5 | OBEDIJULIUS ABELL | NYUMBA | HATIVA MAUZIANO | NGARAMTONI ILIKIUSHIN ARUSHA | 10 NOV. 2021 SAA6 MCHANA |
| 6 | FABIAN KALIST ONNA | NYUMBA | HATIVA MAUZIANO | KISONGO OLISINONI | 11 NOV. 2021 SAA6 MCHANA |
| 7 | MATHIAS PASCAL MASANJA | BOMA | HATIVA MAUZIANO | PLOT NO 1052 BLOCK D MANYONI | 13 NOV. 2021 SAA 5 ASUBUHI |
| 8 | MATHIAS PASCAL MASANJA | BOMA | HATIYA MAUZIANO | PLOT NO 1632 BLOCK KALOLENI MANYONI | 13 NOV. 2021 SAA8 MCHANA |
| 9 | SALUM MACHEMBE NDUSHI | BOMA | HATIYA MAUZIANO | PLOT NO 247 BLOCKCC MANYONI | 14 NOV. 2021 SAA6 MCHANA |
| 10 | MENAS MASENGO | NYUMBA | TITTLE 42032 LO. 242461 | PLOT NO BLOCK IRINGA | 17 NOV. 2021 SAA6 MCHANA |
| 11 | ALFRED ANDREA MLELWA | NYUMBA | HATIYA MAUZIANO | PLOT NO BLOCK NJOMBE | 19 NOV. 2021 SAA6 MCHANA |
| 12 | DANIEL ABIHUDI MWEMBE | NYUMBA | TITTLE NO 4382 LO.97480 | PLOT N 351 BLOCK R SUMWAWANGA | 22 NOV. 2021 SAA6 MCHANA |
| 13 | REINFRIDA SKEETER &EMMANUEL MMBANDO | NYUMBA | TITTLE NO 42032 LO. 142461 | PLOT NO 762 BLOCK A KIJITONYAMA | 26 NOV. 2021 SAA6 MCHANA |
| 14 | REINFRIDA SKEETER ANDEMMANUEL MMBANDO | FARM | TITTLE 17147 LO. 171384 | FARM NO. 860 SHASHUI-SONI LUSHOTO | 30 NOV. 2021 SAA6 MCHANA |
| 15 | BONIFACE VICENT CHAMI | NYUMBA | TITTLE 28870 L0.417827 | PLOT NO 75 BLOCK L NYAKATO | 05 DEC. 2021 SAA6 MCHANA |

**MASHARTI VA MNADA**

1. MNADA UTAFANYIKA SEHEMU DHAMANA ILIPO
2. MNUNUZI ATALAZIMIKA KULIPA 25% YA BEI YA HAPO NA 75% NDANI YA SIKU 14 BAADA YA MNADA
3. ENDAPO MTEJA ATASHINDWA KULIPA NDANI YA SIKU 14 KIASI KILICHOLIPWA AWALI HAKITARUDISHWA NA MNADA UTARUDIWA
4. GHARAMA ZA KUBADILI HATI MILIKI NI JUU YA MNUNUZI MWENYEWE

**KWA MAWASILIANO PIGA NO:-**
0713 604044/ 0688 686905
0766 202191/ 0759 833833

116625901


# Mganga jela miaka 30 kubaka mke wa rafiki

**Na Waandishi Wetu,** PEMBA

MAHAKAMA ya Mkoa B Chakechake imemuhukumu mganga wa kienyeji kifungo cha miaka 30 jela baada ya kupatikana na hatia ya kumbaka mke wa rafiki yake.

Sambamba na kifungo hicho, mahakama imemwamuru kumlipa mwathirika fidia ya Sh. milioni moja.

Mganga huyo, Issa Abdalla Haji (41) mkazi wa Wawi Wilaya ya Chakechake, amehukumiwa kifungo hicho baada ya kukubali kosa hilo.

Akisomewa shtaka na Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Ali Amour Makame, mshtakiwa alikubali kutenda kosa hilo na kuiomba mahakama impunguzie adhabu.

"Mshtakiwa ulimbaka mwanamke baada ya kumwaminisha kwamba wewe ni mganga wa kienyeji utakayemfanyia dawa ya kumtoa mume wake ambaye yuko rumande anayeshtakiwa katika kesi ya jinai namba 140/2021, kosa la wizi wa kutumia silaha, jambo ambalo ni kosa kisheria," alidai mwendesha mashtaka kisha mshtakiwa kukubali kosa.

Hakimu Luciano Nyengo, baada ya mshtakiwa kukubali kosa, alimwamuru kwenda chuo cha mafunzo (jela) miaka 30 na kumlipa mwathiriwa.

Kwa mujibu wa maelezo ya hakimu huyo, mshtakiwa alikuwa rumande na rafiki yake, ikiwa yeye anakabiliwa na tuhuma za wizi huku rafiki yake akikabiliwa na tuhuma za wizi wa kutumia silaha.

"Walipokuwa rumande rafiki yake alimwambia amwambie mke wake akamchukulie dhamana ili na yeye akitoka akamwambie mke wake akamchukulie dhamana," alisema hakimu.

Alisema baada ya mganga huyo kupata dhamana, alikwenda moja kwa moja kwa mke wa rafiki yake na kumwambia akamchukulie mumewe dhamana huku akimpa masharti ya uganga.

"Alimwambia ili mume wako apewe dhamana, lete nywele za sehemu za siri za mbele pamoja na mbegu za kiume, akimaanisha wafanye mapenzi ili wapate hizo mbegu za kiume," alisema Hakimu.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, mshtakiwa alitenda kosa hilo Oktoba 11, mwaka huu, saa 12:00 jioni Wawi, Chakechake, kwa kumbaka mwanamke huyo bila ridhaa baada ya kumwaminisha kwamba atamfanyia dawa ya kumtoa mume wake rumande.

Kufanya hivyo, kwa mujibu wa hati ya mashtaka, ni kosa kinyume na kifungu cha 108 (1), (3),(d), na 109(1) cha Sheria ya Adhabu, Nambari 6 ya mwaka 2018, Sheria ya Zanzibar.

**"Walipokuwa rumande rafiki yake alimwambia amwambie mke wake akamchukulie dhamana ili na yeye akitoka akamwambie mke wake akamchukulie dhamana," alisema hakimu.**


## TANGAZO TANGAZO TANGAZO

JOSINA COMPANY LIMITED NA MOPEH COMPANY LIMITED WATAENDESHA MINADA YA HADHARA YA KUUZA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU WA LETSHEGO BANK TANZANIA LIMITED KUANZIA 22/10/2021 HADI 05/11/2021 MUDA NI KUANZIA SAANNE ASUBUHI NA KUENDELEA

| NA | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA | JINA LA DALALI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | JOHN BHOKE GENTEGAI | GARI NO.T384 BBA LAND CRUISER PRADO | TARIME | | JOSINA CO LTD |
| 2. | PATRICK MWITA NYASWE | GARI NO T.380 BRN LAND CRUISER PRADO | BUZURUGA MWANZA | | JOSINA CO LTD |
| 3 | WEREMA NYAMHANGA MASSANA | NYUMBA(plot NO1957 Block' A' Nyamadoke | BUSWELU MWANZA | | JOSINA CO.LTD |
| 4. | MUSSAYUSUPH MABAWA/ MUSTAPHA R. MUHOGO | NYUMBA Plot NO 321 BLOCK' A' BUSWELU | BUSWELU MWANZA | | JOSINA CO.LTD |
| 5. | JOSEPHAT E. MARWA/ WEMA H. GILALA | KIWANJA (Plot NO 218 block' x' capripoint | CAPRIPOINT MWANZA | | JOSINA CO.LTD |
| 6. | OMARY MOHAMED ATHUMAN/ JACOB STEPHEN LAIZER | NYUMBA MBILI ZIKO KWENYE KIWANJA KIMOJA (plot NO 59 BLOCK' HH' Ndala -shinyanga | NDALA 'B' SHINYANGA | | JOSINA CO.LTD |
| 7. | PAUL NGWELLE DOTTO | NYUMBAPlot NO 109 Block' B' Jiwe kuu | JIWE KUU KITANGIRI MWANZA | | JOSINA CO.LTD |
| 8. | 2M INVESTMENTS LIMITED/ DONATA L.NYALU | NYUMBA Plot NO 248 Block 'A' Kabuhoro | KABUHORO MWANZA | | JOSINA CO.LTD |
| 9. | FADHANA SEIF SENKUNI/ WEMA H. GILALA | NYUMBA Plot NO 57 BLOCK ' I' Bugarika | BUGARIKA MWANZA | | JOSINA. CO LTD |
| 10 | FATMA CHIZENGA | NYUMBA Land no.KDN/MZSUZR/43 | MANZESE-UZURI | | MOPEH COMPANY LIMITED |

**MASHARTI YA MNADA;**

1. DHAMANA ZITAUZWA KAMA ZILIVYO, MNUNUZI ATALIPIA 25% YA BEI YA MNADA. 75% ITALIPWA NDANI YA SIKU 14 KUTOKA SIKU YA MNADA. AKISHINDWA KULIPA, MALIPO YA AWALI HAYATARUDISHWA.
2. GHARAMA ZA KUBADILISHA HATI ZA UMILIKI ZITAKUWA JUU YA MNUNUZI.
3. UKAGUZI WA DHAMANA ZINAZOUZWA UTAANZA SIKU MOJA KABLA YA MNADA NA GHARAMA ZA KUMPELEKA MTEJA KWENYE DHAMANA ZITAKUWA JUU YA MTEJA.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:-**

**MKURUGENZI Josina Co. Ltd: 0768 203 040, WHATSAPP NO: 0713 203 040**
**MKURUGENZI Mopeh Co. Ltd: 0785 335544, WHATSAPP NO: 0785 335544**

116625301

# Hakimu akwamisha hukumu kina Aveva

**Na Kulwa Mzee**

ALIYEKUWA Rais wa Klabu ya Simba, Evans Aveva na Makamu wake, Godfrey Nyange, maarufu Kaburu, jana walitumia muda mwingi kukaa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakisubiri hukumu ambayo imeahirishwa kwa mara ya pili.

Hukumu hiyo ilipangwa kusomwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, kuanzia saa tatu asubuhi lakini walipoingia, iliahirishwa hadi saa nane mchana kwa sababu hakimu alikuwa anamalizia kuandika.

Washtakiwa hao pamoja na Wakili wao, Kung,'e Wabeya, waliingia mahakamani saa nane lakini hukumu haikusomwa kwa sababu Hakimu Simba alikuwa hajamaliza kuandaa hukumu hiyo.

Ilikuwa mara ya pili kwa mahakama hiyo kuahirisha kusoma hukumu hiyo ambapo mara ya kwanza ilikuwa isomwe Oktoba 6, mwaka huu ikaahirishwa hadi jana ambapo pia iliahirishwa hadi Oktoba 28, mwaka huu.

Upande wa mashtaka katika kesi hiyo ulikuwa na mashahidi 10 na upande wa utetezi mashahidi wawili ambao ni washtakiwa, walijitetea wenyewe.

Katika kesi hiyo washtakiwa walikuwa watatu; Aveva, Kaburu na Zackaria Hanspope ambaye alifariki Septemba 10, mwaka huu na hivyo mahakama kuamuru aondolewe katika kesi.

Washtakiwa hao walikuwa wakikabiliwa na mashtaka saba, likiwamo la matumizi mabaya ya madaraka.

Katika shtaka ya kwanza, Aveva na Kaburu wanadaiwa kula njama ya kutenda kosa la matumizi mabaya ya madaraka.

Mshtakiwa Aveva na Kaburu wanadaiwa kutumia vibaya madaraka yao kwa kuandaa fomu ya kuhamisha fedha Dola za Marekani 300,000 kutoka kwenye akaunti ya Simba iliyoko Benki ya CRDB Azikiwe kwenda kwenye akaunti binafsi ya Aveva iliyoko Benki ya Barclays.

Aveva na Kaburu wanadaiwa kwa pamoja walighushi nyaraka zilizokuwa zikionyesha Simba inalipa mkopo wa Dola za Marekani 300,000 kwa Aveva kitu ambacho sio kweli.

Aveva anadaiwa katika Benki ya CRDB kutoa nyaraka ya uongo ikionyesha Simba wanalipa mkopo wa Dola za Marekani 300,000.

Aveva anadaiwa kuwa katika Benki ya Baclays Mikocheni, alijipatia Dola za Marekani 187,817 wakati akijua zimetokana na kughushi.

Kaburu anadaiwa kumsaidia Aveva kujipatia Dola za Marekani 187,817 kutoka kwenye akaunti ya Simba wakiwa wanajua fedha hizo zimetokana na zao la kughushi.

Aveva, Kaburu na marehemu Hans Poppe walikuwa wanadaiwa kughushi hati ya malipo ya kibiashara wakionyesha kwamba nyasi bandia zilizonunuliwa na Simba zina thamani ya Dola za Marekani 40,577 huku wakijua kwamba sio kweli.

Aveva anadaiwa kuwasilisha hati ya malipo ya kibiashara ya uongo kwa Levison Kasulwa kwa madhumuni ya kuonyesha Simba wamenunua nyasi bandia zenye thamani ya Dola za Marekani 40,577.



Aliyekuwa Rais wa Klabu ya Simba, Evans Aveva (katikati), akiwa na jamaa zake akitoka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya hukumu ya kesi inayomkabili kuahirishwa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serengeti yashinda Tuzo Hifadhi Bora

**Na Salome Kitomari**

HIFADHI ya Taifa Serengeti imeshinda tuzo ya hifadhi bora inayoongoza Afrika kwa mwaka 2021, iliyotolewa na World Travel Awards (WTA).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi- Mawasiliano wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Paschal Shelutete, Serengeti imeshinda tuzo hiyo kwa mara ya tatu ikiwa ya kwanza mwaka 2019 na ya pili mwaka 2020.

Alisema Serengeti ina eneo la kilomita za mraba 14,763 ikiwa na utajiri wa wanyama, ndege na uoto wa asili wa aina mbalimbali. "Kuna nyumbu wahamao milioni 1.5, pia ina idadi kubwa ya simba, kuna mwonekano mzuri na urahisi wa mazingira ya asili," alisema.

Shelutete alisema alitaja wanyama wanaonekana kwa makundi makubwa hifadhini humo ni nyumbu wa bluu, swala, pundamilia na nyati.

"Alisema asilimia 70 ya wanyama wazao na aina 500 za ndege wanapatikana hifadhini humo hali inayochangia uwepo wa tabia tofauti, na kuna mito, mabwawa, maeneo oevu, nyasi na misitu.

"TANAPA inatambua na kuthamini mchango kutoka serikalini, Watanzania, wadau wa utalii na wale waliotenga muda kupiga kura kwa kivutio hicho," alisema.

Hifadhi zingine zilizoshinda ni Pori la Akiba Central Kalahari (Botswana), Hifadhi ya Taifa Etoshi (Namibia), Hifadhi ya Taifa Kidepo Valley (Uganda), Hifadhi ya Taifa Kruger (Afrika Kusini) na Pori la Akiba Masaai Mara la Kenya.

## Mume na mke wauawa wakiwa wamelala usiku

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATU wawili, mke na mume, Anes Haule (45) na Menluph Ngailo (45) wameuawa kwa kukatwa katwa mapanga wakiwa wamelala nyumbani kwao katika kijiji cha Itacha, Ludewa mkoani Njombe.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, alisema tukio hilo lilitokea Oktoba 19, mwaka huu, majira ya saa 2:00 usiku.

"Hawa wanandoa wakiwa nyumbani kwao, walivamiwa na watu wakiwa na silaha zenye ncha kali na waliwasababishia majeraha kichwani, shingoni, mashavuni, begani na majeraha haya ndiyo yamesababisha kufariki dunia," alisema.

Kamanda Issa alisema Jeshi la Polisi liliingia kazini na kubaini watuhumiwa wa tukio hilo ambao ni wanandugu wawili na kuwakamata.

"Baada ya vielelezo fulani vinavyohusiana na uchunguzi kuonekana kuwa wamehusika ni wanandugu wa kike na wa kiume ambao wa kwanza Nuru Ngailo na wa pili ni Evanjelista Ngailo, huyu ni dada wa marehemu, hawa walikuwa wanamtuhumu ndugu yao kuwa ni mshirikina kwa sababu wao walikuwa wakiishi katika mazingira ya kuumwa umwa wakasema wanarogwa na huyo kaka yao, wakishirikiana na mke wake," alisema.

Kamanda alisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi ili kujua ukweli wa jambo hilo ili sheria ifuate mkondo wake.

Pia amewaasa wananchi kuachana na imani za kishirikina kwa madai kwamba zimepitwa na wakati.

**"Hawa wanandoa wakiwa nyumbani kwao, walivamiwa na watu wakiwa na silaha zenye ncha kali na waliwasababishia majeraha kichwani, shingoni, mashavuni, begani na majeraha haya ndiyo yamesababisha kufariki dunia," alisema.**

## HABARI KITAIFA



Mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Buhongwa A, jijini Mwanza, Eliya Yohana akiwa amebebwa juu na wanafunzi wenzake jana, baada ya kuibuka mshindi wa shindano la mchoro wa usalama barabarani linayoendeshwa na kampuni ya Puma Energy kupitia programu yake ya kutoa mafunzo ya elimu ya usalama barabarani kwa kushirikiana na Amend, na kujinyakulia kombe, cheti na kitita cha 500,000/- pia kuiwezesha shule hiyo kupata Sh. milioni nne. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Meneja TARURA mtegoni ujenzi daraja

**Na Thobias Mwanakatwe,** MBOZI

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, ametoa siku saba kwa Meneja wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) Wilaya ya Mbozi, Mhandisi Naftari Chaula, kukamilisha ujenzi wa daraja linalounganisha vijiji vya Idiwili na Ilomba kwenye Mto Songwe.

Alitoa agizo hilo jana baada ya kukagua daraja hilo na kupokea malalamiko ya wananchi juu ya kusuasua kwa ujenzi, ikiwa ni siku ya kwanza ya ziara yake ya siku nne ya kukagua shughuli za maendeleo katika wilaya ya Mbozi.

Mgumba alisema mkandarasi wa mradi huo, ambaye ni kampuni ya Lumo kutoka Dar es Salaam, tayari alishalipwa fedha zote kwa mujibu wa mkataba, hivyo kitendo cha mradi huo kushindwa kukamilika kwa wakati ni uzembe ambao hauvumiliki.

"Natoa ahadi kama kiongozi mkuu wa mkoa huu kwamba hatukuja hapa kufanya sanaa au kiini macho na ndani ya siku saba kama daraja hili halijakamilika, nimemwambia injinia hapa atafute kazi nyingine," alisema.

Mgumba alisema kwa mujibu wa mkataba, mkandarasi huyo alitakiwa kumaliza ujenzi wa daraja hilo Januari, mwaka huu, lakini aliomba nyongeza ya muda hadi Septemba 30, mwaka huu.

"Wananchi naomba muwe na imani na serikali yenu maana hatukuja kubembelezana hapa kwa kuwa mkandarasi alishapewa fedha zote na muda wa nyongeza alioomba ili amalizie kazi umeisha," alisisitiza Mgumba.

Kabla ya mkuu wa mkoa kutoa agizo hilo, mmoja wa wananchi wa Kijiji cha Ilomba, Jumamosi Shikombo, akiuliza swali alitaka kujua sababu zinazosababisha ujenzi wa daraja hilo kusuasua na kusababisha adha na wananchi kuhatarisha maisha yao kwa kupita kwenye kivuko kilichojengwa kienyeji.

Alisema kivuko kinachotumika kwa sasa ni hatari kwa usalama wa watumiaji hususani kipindi hiki amabacho mvua za msimu zinatarajia kuanza kunyesha.

Naye Meneja wa TARURA Wilaya ya Mbozi, Mhandisi Chaula alisema muda uliotolewa na mkuu wa mkoa unatosha kukamilisha mradi huo.

Mhandisi Chaula alisema mbali na daraja hilo, serikali imetenga Sh. milioni 134 kwa ajili ya kuiimarisha barabara hiyo ya Idiwili -Ilomba yenye urefu wa kilometa saba kwa kujenga kwa kiwango cha changalawe.

# RC ahamasisha wanahabari chanjo corona

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joseph Mkirikiti, amewataka waandishi wa habari mkoani hapa kupata chanjo ya corona kwa kuwa wako katika makundi hatari kutokana na kukutana na watu wengi wanapokwenda kutekeleza majukumu yao.

Ushauri huo aliutoa jana wakati anazungumza na waandishi wa habari mjini hapa akielezea mafanikio ya serikali ya awamu ya sita katika kipindi cha miezi sita tangu ilipoingia madarakani. Alisema waandishi wa habari ni kundi lililo katika hatari ya kupata ugonjwa wa corona kwa sababu wamekuwa wakikutana na wananchi wengi pamoja na viongozi mbalimbali, hali inayowaweka katika hatari ya kupata ugonjwa huo.

"Nawashauri waandishi wa habari na ninyi mchanje maana mko katika makundi hatari. Mnapofanya kazi zenu mnakutana na wananchi wengi na mnakutana na viongozi pia. Kwa maana hiyo salama yenu ni kuhakikisha mmechanja na kufuata taratibu zote za kujikinga kama zinazoelekezwa na wataalamu wa afya," alisema.

Pia alisema tayari mkoa umetoa chanjo zote 20,000 ambazo serikali ilitoa kwa awamu ya kwanza na sasa mkoa umepokea chanjo zingine 24,000 kwa ajili ya wananchi kuendelea kuchanja.

Alisema chanjo hizo zitakuwa zikitolewa kuanzia ngazi ya kitongoji ili wananchi wengi zaidi wafikiwe na wasilazimike kusafiri umbali mrefu kufuata chanjo katika vituo vilivyowekwa.

Mkirikiti pia aliwataka waandishi wa habari kutumia vyombo vya habari hasa redio za mkoani hapa kuhamasisha wananchi wajitokeze kwa wingi kupata chanjo hiyo kwa kuwa zipo na zinatolewa bure katika maeneo yaliyoainishwa kwa ajili ya kupeleka chanjo hiyo.


## SAO HILL ENERGY LIMITED

The companies Act, 2002 (Section 334)
**MEMBER'S VOLUNTARY WINDING – UP**
**NOTICE IS HEREBY GIVEN** to the general public that **SAO HILL ENERGY LIMITED** a company with registration number **40027** dully convened a meeting on 14th July, 2021 and passed a special resolution in accordance to section 333 (1) (b) of the Companies Act, 2002 that the company be wound up voluntarily.

All parties concerned and who have claims are hereby notified to submit their claims in a closed envelop within 30 days to **GODFREY BASIL MRAMBA of Basil & Alred, Ace Building, Haile Selassie Road, P.O. Box 78661, Dar es salaam, Tanzania,** who is appointed Liquidator of the Company.

**Any claims lodged after 30 days from this publication will not be considered for admission.**

**GODFREY BASIL MRAMBA**
**Liquidator**
**For SAO HILL ENERGY LIMITED**

116525001

SAO HILL ENERGY LIMITED

REG: 40027

EXTRACT FROM THE MINUTES OF THE EXTRA - ORDINARY GENERAL MEETING OF SAO HILL ENERGY LIMITED HELD AT ITS REGISTERED OFFICE

ON 14 JULY 2021 AT 13:00 P.M

**MEMBERS PRESENT WERE:**

1. **GODLISTEN MINJA** — **DIRECTOR/ CHAIRMAN**
2. **LILIAN KITOSY** — **DIRECTOR**
3. **ANNETTE KIRETHI** — **COMPANY SECRETARY**

**THE CHAIRMAN REPORTED** that according to the Company activities, the Shareholders of **SAO HILL ENERGY LIMITED** (hereinafter called "the Company") is desirous of voluntarily winding up the Company.

SPECIAL RESOLUTIONS

**IT WAS RESOLVED**

1. That, the Company be voluntarily liquidated and dissolved as decided by members;
2. That, Godfrey Basil Mramba be and is hereby appointed as a liquidator for the purpose of winding up the affairs and distributing the assets of the Company.
3. That, the remuneration payable by the Company to shall be negotiated and agreed based on the man-hour spent on this assignment;
4. That **M/S Basil & Alred** be and is hereby appointed auditor for the purpose of auditing the Liquidator's account of the winding up of the affairs of the Company;
5. That the remuneration payable by the Company to **M/S Basil & Alred** as auditor shall be negotiated and agreed based on the man-hour spent on this assignment.

The above is a certified True Copy of
The Resolution of theBoard of Directors

**CHAIRMAN** **COMPANY SECRETARY**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Tuitumie vizuri fursa iliyoletwa na Ufaransa

**HIVI** karibuni Waziri wa Mambo ya Nje, Biashara na Vivutio vya Kiuchumi wa Ufaransa, Franck Reister, alikuja nchini na ndege ya Shirika la Air France ya moja kwa moja kutoka Paris, Ufaransa hadi Zanzibar.

Ujio wake huo uliambatana na uzinduzi wa rasmi wa safari za ndege za shirika hilo za Ufaransa-Zanzibar, viongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakishiriki.

Waziri huyo pia alizuru Dar es Salaam katika Ubalozi wa Ufaransa nchini na kuona magari yanayotengenezwa na kampuni moja kutoka nchini humo ambayo yana mfumo wa umeme, yakielezwa kuwa ni rafiki kwa mazingira kwa kuwa hayana kelele na hayatoi hewa ukaa ambayo huchangia mabadiliko ya tabianchi.

Tayari Kampuni ya Utalii ya Mount Kilimanjaro Safari Club inatumia magari hayo kusafirisha watalii, magari hayo yakitengenezwa kwa ushirikiano kati ya kampuni ya Ufaransa na Tanzania, huku kukiwa na ushirikishwaji wa teknolojia.

Waziri huyo pia alikutana na mawaziri wanne wa sekta za uwekezaji, nishati, usafirishaji na mambo ya nje pamoja na kampuni ya Kifaransa nchini na wafanyabiashara mbalimbali kujadili namna ya kuendelea kushirikiana kwa manufaa ya nchi zote.

Kiongozi huyo wa Ufaransa pia alikutana kwa mazungumzo na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, yote ikiwa ni namna ya kuimarisha ushirikiano baina ya nchi hizo mbili ambazo kwa miaka mingi zimekuwa na uhusiano wa kidiplomasia.

Viongozi hao wakashiriki uzinduzi wa duka la kisasa la bidhaa mbalimbali kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Terminal Three, ambayo yanamilikiwa na kampuni za Ufaransa na Tanzania, ambayo yametoa ajira kwa Watanzania.

Kuanza upya kwa safari za ndege za moja kwa moja kutoka Paris, Ufaransa hadi Tanzania ni hatua kubwa katika sekta ya utalii kwa kuwa mara ya mwisho ndege hiyo kuja nchini ilikuwa mwaka 1974, yaani miaka 47 iliyopita.

Nipashe tunaamini ushirikiano huo utanufaisha pande zote, kwamba wakati kampuni za Ufaransa zikija kuwekeza nchini, Watanzania waone fursa za uwekezaji kwenye nchi hiyo au kujifunza ubunifu na teknolojia katika kuleta mabadiliko kwao.

Hakuna ubishi Ufaransa ni moja ya nchi zilizoendelea si tu kiteknolojia, bali pia kiuchumi duniani, yapo mengi ya Tanzania itajifunza kutoka taifa hilo la Bara la Ulaya kwa kadri ya maudhui na mahitaji ya nchi, lakini kulinda mila na tamaduni kusije kusahaulika.

Tunaamini ushirikiano huo ni fursa ya ajira katika sekta mbalimbali ikiwamo utalii kwa kuwa ujio wa watalii kwa wingi nchini unapaswa kwenda sambamba na kuzalisha rasilimali watu ya kuitumikia sekta ya utalii, hivyo Watanzania wengi watapa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja.

Ni wajibu wa serikali kwa kushirikiana na taasisi zake na sekta binafsi kuwa na mkutano wa pamoja kujadili kwa kina ushirikiano huo sambamba na kuwajengea uwezo wananchi namna ya kuziona fursa mbalimbali za nje ya nchi kwa manufaa yao binafsi na taifa kwa ujumla.

Tunatarajia kuona kumiminika kwa kampuni za nchi hiyo kuwekeza nchini kunakwenda kuwanufaisha wananchi wengi, badala ya maslahi ya mtu mmoja.

Nipashe tunaamini ni aibu nchi kuwa na raslimali na utajiri mwingi lakini raia wake hawaoni umuhimu wake kwa kuwa tu kuna viongozi waliingia mikataba ambayo haikuzingatia maslahi mapana ya nchi.

Ni katika muktadha huo, Nipashe tunaona kuna haja Tanzania kuchangamkia fursa iliyoletwa na Ufaransa nchini wakati huo wakiwa na hadhari katika uamuzi wowote unaogusa maslahi ya Watanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

# Machinga Dar tumieni vizuri siku 12 za rehema mlizopewa

Na Sabato Kasika

**TANGU** tarehe 18 ya mwezi huu, baadhi ya machinga wa Dar es Salaam waliondoka maeneo waliokuwa wakifanyia biashara, kwa kutii maelekezo ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, aliyetaka kufikia tarehe hiyo wahame.

Hata hivyo, ameamua kuwaongezea siku nyingine 12, kwa lengo la kuwapa muda zaidi wa kuhamisha bidhaa zao kwenda kule ambako wamepangiwa ili kuendelea na shughuli zao kama kawaida.

Kwa kuwa zimeongezwa siku zaidi kabla ya kuhama, ni vyema kama machinga wangetumia nafasi hiyo kuhakikisha wanaondoa bidhaa zao vizuri na kwenda kule walikopangiwa badala ya kusubiri siku ya mwisho.

Mfano mzuri ni wale ambao tayari wamehama wakitambua kile ambacho wameelekezwa, wanajua kuwa si vyema kusubiri kuhama kwa shuruti na ingependeza kama wote wangefuata utaratibu huo.

Lengo la serikali kama lilivyoelezwa na Rais Samia Suluhu Hassan, ni kuwapanga ili wafanye biashara kistaarabu kuliko ilivyo sasa, baadhi wapo katika hifadhi ya barabara na wengine kwenye mitaro ya maji ya mvua. Inawezekana wakatokea wachache wa wanaotaka kukwamisha uhamaji huo kama ilivyotokea Kariakoo, baada ya kuibuka kundi lililotaka kuzuia viongozi wa machinga waliokuwa wakiwapanga wafanyabiashara.

Kinachofanywa na serikali ni kutaka machinga wanafanye biashara zao katika mazingira rafiki, ambayo watakuwa salama na pia kutochafua mazingira, kuhatarisha afya zao na kutobughudhi watumiaji wengine wa barabara.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba, baadhi yao wamekuwa wakichangia katika kuchafua mazingira kwa kutupa ovyo taka wanazozalisha na wakati kujisaidia haja ndogo katika mitaro ya kupitisha maji ya mvua.

Kimsingi, mtindo huo pamoja na ule wa baadhi ya mama lishe na baba lishe kuandalia vyakula barabarani au vichochoroni, si ya kistaarabu na ni vyema wakabadilisha mazingira hayo kama ambavyo serikali inataka wafanye.

Lakini kwa kuwa uzoefu unaonyesha kila machinga wanapohamishwa, umekuwa ukitokea mvutano kati yao na vyombo vya dola, ingekuwa vyema iwapo uhamaji huo hautakumbana na hali kama hiyo.

Binafsi ninaamini serikali ina nia njema ya kutaka machinga waendeshe shughuli zao katika maeneo ambayo ni rasmi, bila kuhatarisha usalama wao au kuchafua mazingira kama imejitokeza kwenye baadhi ya maeneo.

Mfano ambao baadhi ya machinga wa Dar es Salaam wameuonyesha wa kuondoka wenyewe bila shuruti, ungeigwa na wengine wanaosubiri hadi kumalizika kwa siku 12 zilizoongezwa na mkuu wa mkoa.

Katika tathmini yake, mkuu wa mkoa anasema uhamaji unakwenda vizuri na kwamba siku 12 alizoongeza anaamini hakutakuwa na mfanyabiashara atakayekuwa amebaki kwenye eneo lisilo rasmi.

Maana yake ni kwamba, anatarajia kuwa machinga hawatamwangusha, pia anajiandaa kusimamia sheria ili kuhakikisha hakuna machinga atakayerejea kwenye eneo aliloondolewa.

Hivyo kauli hiyo ingechukuliwa kwa uzito na machinga wenyewe kwa kuwa anasema, kwa mujibu wa kanuni zake, ni marufuku kufanya biashara yoyote katika hifadhi ya barabara ambapo faini yake ni Sh. 300,000 au jela miaka mitatu ama vyote kwa pamoja.

Anabainisha kuwa, serikali inawapenda, ndiyo maana imeamua kuwaondoa ili wasitozwe faini au kufungwa, hivyo ni vyema watumie muda walioongezewa kuhakikisha wanatii kile walichoelekezwa.

TANGAZO

BancABC part of atlasmara

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED
### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 30-Sep-21 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 30-Jun-21 |
|---|---|---|---|
| **A** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 6,574 | 4,762 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 14,624 | 9,864 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 43,837 | 42,827 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 4,576 | 5,883 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 104,375 | 105,943 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 127,516 | 125,435 |
| | | - | - |
| 12 | Mali Nyingine | 25,094 | 25,783 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,000 | 1,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 8,768 | 6,827 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **336,365** | **328,325** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 91,519 | 101,584 |
| 18 | Amana za Wateja | 129,815 | 110,991 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 2,052 | 1,464 |
| 28 | Madeni | 77,093 | 76,856 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **300,479** | **290,894** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **35,885** | **37,431** |
| **C** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 122,954 | 122,954 |
| 32 | Hifadhi isiyosambazwa | 1,716 | 1,716 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (86,263) | (86,263) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (3,511) | (1,965) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 989 | 989 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **35,885** | **37,431** |
| | | - | - |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 3,680 | 2,374 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 18,575 | 19,109 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 13,011 | 12,796 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 10.67% | 11.40% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 13.22% | 13.82% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 63.49% | 65.03% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 37.91% | 38.20% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 48.03% | 49.18% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 4.12% | -1.21% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 2.45% | -0.90% |

### AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED
### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-21 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita 30-Sep-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-20 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 10,246 | 11,191 | 30,311 | 32,078 |
| 2 | Gharama za Riba | (5,190) | (5,113) | (14,976) | (14,542) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **5,057** | **6,078** | **15,335** | **17,537** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 206 | 439 | 319 | 1,294 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | - | - | (520) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,163** | **940** | **3,454** | **2,856** |
| 6.1 | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 192 | 349 | 699 | 1,052 |
| 6.2 | 6.2 Ada na Kamisheni | 249 | 400 | 682 | 750 |
| | 6.3 Gawio | 35 | - | 35 | - |
| 6.3 | 6.4 Mapato Mengine | 687 | 191 | 2,038 | 1,054 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(7,961)** | **(8,040)** | **(22,496)** | **(22,665)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,510) | (2,567) | (7,608) | (7,588) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (5,451) | (5,473) | (14,888) | (15,077) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(1,535)** | **(583)** | **(3,388)** | **(1,498)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (10) | (34) | (122) | (101) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(1,545)** | **(617)** | **(3,511)** | **(1,600)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(1,545)** | **(617)** | **(3,511)** | **(1,600)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 168 | 153 | 168 | 153 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (0.63) | (0.00) | (0.36) | (0) |
| 15 | Mapato yaliyopatikana kwa Kushiriki | - | - | - | - |
| 16 | Idadi ya Matawi | 6 | 6 | 6 | 6 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | 0 | - | 0 | - |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -0.62% | -0.26% | -2.11% | -0.67% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -5.62% | -1.94% | -19.15% | -5.04% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 128.72% | 114.56% | 119.96% | 111.14% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 0.96% | 1.19% | 2.92% | 3.44% |

### AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED
### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | 30-Sep-21 | 30-Jun-21 |
|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (1,535) | (1,134) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 776 | 803 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (2,080) | 4,778 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 8,760 | (2,605) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (1,011) | 1,324 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 588 | (378) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 689 | 1,191 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (10) | (19) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **6,177** | **3,960** |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (2,716) | (1,399) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(2,716)** | **(1,399)** |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 237 | 1,150 |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **237** | **1,150** |
| | | - | - |
| **IV** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 3,697 | 3,711 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 126,452 | 122,741 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **130,149** | **126,452** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2021

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 122,954 | - | (86,262) | 1,716 | 0 | 989 | 39,396 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (3,511) | - | - | - | (3,511) |
| Hisa za upendeleo | - | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 122,954 | - | (89,773) | 1,716 | 0 | 989 | 35,885 |
| | - | - | - | - | - | - | 0 |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 122,954 | - | (80,525) | 130.00 | 0 | 1,065 | 43,623 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (4,152) | - | - | - | (4,152) |
| Hisa za upendeleo | - | - | - | - | - | - | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (1,586) | 1,586 | - | (76) | (76) |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 122,954 | - | (86,262) | 1,716 | 0 | 989 | 39,396 |

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Ofisa Mtendaji Mkuu | I. John | | 22nd October 2021 |
| Mkuu wa Fedha | H. Kharbush | | 22nd October 2021 |
| Mkaguzi Mkuu wa Ndani | J. Kilato | | 22nd October 2021 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mkurugenzi | P. Ishengoma | | 22nd October 2021 |
| 2 | Mkurugenzi | Mr.R. Dave | | 22nd October 2021 |

116526301

# Wakanusha kutelekeza watoto kisa ulemavu

**Nusha na Christina Haule,** KILOSA

SUALA la wafugaji wa jamii ya kuhamahama kuacha watoto wenye ulemavu kwenye maboma wakati wakihama kwa madai kuwa ni mzigo usio na faida zaidi ya ndama, imebainika kuwa ni msemo usio na ukweli ndani yake.

Wafugaji wa jamii ya Kimasai walisema hayo jana kuwa ipo misemo ya namna hiyo ikimaanisha kwamba hawana watoto wenye ulemavu kwa sababu ya kuwaacha kwenye maboma yao na kisha kufariki dunia kutokana na kuwa wapweke bali zamani hawakuwa wakipata watoto wenye ulemavu kama sasa.

Mmoja wa wafugaji hao, Farais Makala (70), mkazi wa kijiji cha Twatwatwa wilayani Kilosa, Morogoro, alisema zamani walikuwa hawapati watoto wenye ulemavu labda ulemavu wa mguu au miguu pekee.

Alisema kwa sasa wamekuwa wakipata watoto wenye ulemavu wa aina mbalimbali hata wale wasiokuwa na uwezo wa kutembea kabisa na kwamba wamekuwa wakijitahidi kuwatafutia matibabu kama watu wengine na mpaka walipogundua kituo cha Amani Centre kuwa mkombozi wao kwa watoto kwa kuwapa mazoezi, tiba na lishe.

Makala alisema hata wanaoua wanyama wa pori huishia kwenye dhambi na si maendeleo yoyote kama wanavyopanga bali ni umaskini. “Kuwaacha watoto na kuhama ni dhambi na kama utafanya hivyo, familia nzima itaishia pabaya. Itakuwa sawa na mtu uliyemfukuza kwako na akaenda porini na kuliwa na wanyama wakali, lazima utapata dhambi,” alisema. Aidha, Makala alisema hata wanaosema mwanamume wa Kimasai yeyote anaweza kuchomeka mkuki mlangoni kwa nyumba ya mwenzie na kuingia ndani kupata huduma kwa mke wa mwenzie na mwenyewe akija asifanye lolote, si kweli bali ni maneno na misemo tu ambayo inapaswa kupuuzwa.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Manyara, Kijiji cha Twatwatwa, Parisiato Lamaray, alisema alikuwa na mtoto mwenye ulemavu wa viungo ambaye hakuinuka kabisa na kwamba baada ya tiba na mazoezi kupitia kituo cha Amani, amesimama na ni mchangamfu kama watoto wengine.

Naye Agnes Ngale (24), mama wa watoto watatu, akiwamo mmoja mwenye ulemavu, alisema wamekuwa wakiwabeba watoto wenye ulemavu kama mizigo na kuhama nao pale inapobidi na si kuwatelekeza kama ilivyokuwa zamani. Ngale aliwashauri wanawake wenzie wenye waoto wenye ulemavu kutokata tamaa kuwahudumia watoto wao bali wawapeleke kwenye vituo vya kufanyia mazoezi na kupata tiba sahihi ili nao watembee kama mtoto wake.

Mkurugenzi wa Amani Centre, kituo kinacholea watoto wenye ulemavu wa viungo na akili, Padri Beatus Sewando, alisema wamechagua kutembelea kijiji hicho cha wafugaji ili kuwasaidia kutokana na kuwa na utamaduni wa kutowajali watoto wenye ulemavu.

# BoT yakunwa mfumo wa majaribio kidigitali NMB

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imezindua Mfumo wa Majaribio ya Suluhishi za Kidigitali (Sandbox Environment), ikiutengea Sh. bilioni 1 za kusaidia bunifu zitakazopita, mfumo, ambao umepongezwa na Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dk. Bernard Kibesse.

Kibesse amezitaka taasisi za fedha nchini kuiiga NMB katika kuleta njia mbadala za kutoa suluhu za kibenki ambazo ni rahisi, haraka na salama.

NMB Sandbox ni jukwaa huru la NMB linalotoa fursa kwa wabunifu wa Kidigitali na wabunifu binafsi wa Kitanzania kutumia Mifumo ya Benki ya NMB kujaribu suluhishi zao, kabla ya kuanza kutumika rasmi.

Uzinduzi huo ulifanyika jijini Dar es Salaam jana, ambapo Mgeni rasmi wa tukio kilo Dk. Kibesse alisisitiza kuwa benki nchini hazina budi kuendana na kasi ya mabadiliko ya tekinolojia, ili kutoa suluhishi za huduma za kibenki, hasa katika nyakati hizi, ambazo tekinolojia imetanua wigo wa kuhudumia.

“Uzinduzi huu wa Sandbox Environment, unafungua fursa kwa kampuni changa na wabunifu binafsi kuonyesha ujuzi wao na kubuni suluhishi zitakazopunguza gharama za kibenki kwa watu wote, sambamba na kutengeneza ajira kwa vijana wa Kitanzania.

“BoT inatambua changamoto zinazo wakabili wateja wanapotumia huduma za kibenki, zikiwamo upatikanaji hafifu wa huduma hizo, ufinyu wa njia za kufikisha, gharama na uelewa mdogo walionao katika masuala ya fedha.

“Serikali kupitia BoT imechukua hatua mbalimbali kumaliza changamoto hizo na uzinduzi huu unaashiria kuwa NMB inaunga mkono jitihada hizo, kama ilivyofanya kutenga Sh. Bilioni 100 za mikopo nafuu kwa wakulima, wafugaji na wavuvi,” alisema Dk. Kibese, akiahidi kuwa BoT itaendelea kushirikiana na NMB katika kuboresha sera zinazotoa mwongozo na kurahisisha ufanyaji wa biashara kwenye sekta ya kibenki.

Awali, Afisa Mtendaji Mkuu wa NMB, (CEO), Ruth Zaipuna, alisema benki yake imejizatiti na kujipambanua kuendana na kasi ya tekinolojia kwa kuleta suluhishi mpya zinazorahisisha huduma za kibenki kwa mteja mmoja mmoja na wafanya biashara wadogo na wa kati na kwamba benki yake imetenga kiasi cha Sh. bilioni 1, kwa ajili ya kuziwezesha suluhishi zitakazopita katika majaribio hayo.

Zaipuna alimhakikishia Dk. Kibese kuwa, licha ya kwamba utatumika kwa majaribio, lakini Sanbox Environment hautaathiri kwa namna yoyote usalama wa taarifa, amana na faragha za wateja wao na kwamba baadhi ya tuzo za miaka ya karibuni ilizopata benki hiyo, zimetokana na uwekezaji mkubwa waliofanya katika mifumo ya kidigitali.

“Hivi karibuni tumeshinda Tuzo ya Benki Bora ya Ubunifu ya wateja binafsi kutoka Jarida la Kimataifa la International Banker, huku tukiendelea kuongoza sokoni katika kutoa huduma za kibenki kidigitali na kuongeza bunifu Kama hizi za kuwaleta karibu wateja wetu kupitia mifumo ya kiteknolojia.


BancABC part of atlasmara

## MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| | PRICING (TZS) | PRICING (US $ / EUR) | PRICING (GBP) |
|---|---|---|---|
| **PERSONAL BANKING** | | | |
| **SAVINGS ACCOUNT** | | | |
| **IZZE** | | | |
| Account Opening Fee | Free | NA | NA |
| Opening balance | Free | NA | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NA | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 10,000.00 | NA | NA |
| Monthly Service Fee | Free | NA | NA |
| **FAHARI** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Monthly Service Fee | TZS 1,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| **MWANGAZA JUNIOR ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 20,000.00 | $ 500.00 | £ 500.00 |
| Extra fee for more than 1 w/drawal per quarter | TZS 5,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| Monthly Service Fee (1 free w/drawal per quarter) | Free | Free | Free |
| **WEKEZA SAVINGS ACCOUNT (BALANCE BUILD UP)** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | Free | Free | N/A |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 100,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | N/A |
| **CURRENT ACCOUNT** | | | |
| **AMANA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | N/A | N/A |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | N/A | N/A | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| **MARIDHAWA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 25,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 6,000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **PREMIUM** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 35,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **SME BANKING** | | | |
| **AMANA BIZ ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 50,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| **SME TIERED CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | TZS 1,000,000.00 | $ 1,000.00 | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 5,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 15.00 | NA |
| **JAMII CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | Free | Free | Free |
| Minimum Operating Balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 50,000.00 | £ 50,000.00 |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | Free |
| **CORPORATE BANKING** | | | |
| **CORPORATE CURRENT ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | £ 250.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE CALL ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 1.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE TIERED INTEREST ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000,000.00 | $ 100,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | NA |
| **GENERAL CHARGES** | | | |
| Bankers Cheque | TZS 50,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| DISHONORED/UNPAID CHEQUE | | | |
| Fund related | TZS 120,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| Technical | TZS 30,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| **Cheque book Processing Fee:** | | | |
| 25 leaves | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 50 leaves | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 20.00 |
| 100 leaves | TZS 50,000.00 | $ 35.00 | £ 35.00 |
| Uncollected cheque book after 3 months | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 3rd party encashment (with 3rd party indemnity) | TZS 25,000.00 | 1% Per Cheque + $20 | 1% Per Cheque +$20 |
| Stop Payment Charges | TZS 30,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| **TRANSACTIONAL SERVICE FEES** | | | |
| **With banks via Standing Orders** | | | |
| Standing Order - internal same customer ( set up fee - once off) | Free | Free | Free |
| Standing Order - internal other customers ( per transaction) | Free | Free | Free |
| Standing Order - Other local bank | TZS 20,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Amendment | Free | Free | Free |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS:** | | | |
| Cash Deposit at Branch | Free | Free | Free |
| Cash Deposit at Branch coins above 100,000 | 5% Min 10,000 | NA | NA |
| Cash Deposit at Branch small denominations less than 50USD (USD 1,2,5,10,20) equal and above USD 500 | NA | 3% of FCY currency value | 3% of FCY currency value |
| With Account Transfers (Internal) | Free | Free | Free |
| Cheque deposit | Free | Free | Free |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) up to 2m | TZS 3,500.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) btn 2m to 20m | TZS 4,000.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) above 20m | 0.15% Max 50,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal SME ( over the counter) | 0.15%Min 3,000 Max 20,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Corporate Banking | 0.15%Min 3,000 Max 100,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Deposit charges - Financial Institution. | Free | Free | Free |
| Deposit charges - Financial Institution - small denominations | Free | 3%On small denominations above $500 | 3%On small denominations above $500 |
| Account Closure | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account Reactivation | NIL | NIL | NIL |
| Dormant Account monthly fee | NIL | NIL | NIL |
| Premature/cancellation fixed deposit fee | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited |
| Monthly statements | Free | Free | Free |
| Interim Statements (per page) | TZS 2,000.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Search fee documents (after 3 months) | TZS 80,000.00 | $ 40.00 | £ 40.00 |
| Audit confirmation | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Balance Certificate | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Reference Letter | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Inter Account Transfers | Free | Free | Free |
| T T Outward local - TISS | TZS 11,800.00 | $ 10.00 | N/A |
| T T Outward local - EFT | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| T T Inward local TISS | Free | Free | N/A |
| Salary processing (per entry) | TZS 1,500.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| International Outward T T | N/A | $50 + Other overseas bank chrges | $50 + Other overseas bank chrges |
| International Inward T T | N/A | Free | Free |
| Travellers Chq. Deposit | N/A | N/A | N/A |
| Foreign BankDrafts | N/A | $ 50.00 | £ 30.00 |
| Outward Cheque for Collection | N/A | N/A | N/A |
| Outward Bills for collection | N/A | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) |
| Inward Bills for Collection | N/A | 0.25% MIN 50 | 0.25% MIN 50 |
| Advising fee (Inward Bill & LCs ) | N/A | $ 200.00 | £ 200.00 |
| Travellers Chq. (Issue) | N/A | N/A | N/A |
| Letters of Credit | N/A | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) |
| Bank Guarantees | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 |

## RC: Waandishi changamkieni chanjo UVIKO-19

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joseph Mkirikiti, amewataka waandishi wa habari mkoani humo kuchanja chanjo ya kujikinga na ugonjwa wa UVIKO- 19 kwani wao pia wako katika makundi hatari ya kuambukizwa.

Alisema hali hiyo inatokana na kukutana na watu wengi wanapokwenda tekeleza majukumu yao.

Ushauri huo aliutoa jana wakati anazungumza na waandishi wa habari mkoani humo akielezea mafanikio ya serikali ya awamu ya sita katika kipindi cha miezi sita tangu ilipoingia madarakani.

Alisema kuwa waandishi wa habari ni kundi lililo katika hatari ya kupata ugonjwa wa UVIKO-19 kwani wamekuwa wakikutana na wananchi wengi pamoja na viongozi mbalimbali, hali inayowaweka katika hatari ya kupata ugonjwa huo.

"Nawashauri waandishi wa habari na nyinyi mchanje, maana mmo katika makundi hatari, mnapofanya kazi zenu mnakutana na wananchi wengi na mnakutana na viongozi pia," alisema na kuongeza:

"Kwa maana hiyo salama yenu ni kuhakikisha mmechanja na kufuata taratibu zote za kujikinga kama zinazoelekezwa na wataalamu wa afya."

Aidha, alisema kuwa mkoa huo umefanikiwa kutoa chanjo zote 20,000 ambazo serikali ilitoa kwa awamu ya kwanza na hivi sasa mkoa umepokea chanjo nyingine 24,000 kwa ajili ya wananchi kuendelea kuchanja.

Alisema hivi sasa chanjo hizo zitakuwa zikitolewa kuanzia ngazi ya kitongoji ili wananchi wengi zaidi wafikiwe na wasilazimike kusafiri umbali mrefu kufuata chanjo katika vituo vilivyowekwa.

Aliwataka waandishi wa habari kutumia vyombo vya habari mkoani humo kuhamasisha wananchi wajitokeze kwa wingi kupata chanjo hiyo, kwani chanjo zipo na zinatolewa bure katika maeneo ambapo kunavituo vya kutolea chanjo hizo.

# Jaji ataka ushahidi kesi zinazopelekwa kortini

**Renatha Msungu,** DODOMA

MWENYEKITI wa Chama cha Majaji na Mahakimu Wanawake (TAWJA), Jaji Joaquine De Mello, amewataka wadau wote wa haki wakiwamo wapelelezi kuhakikisha kesi zinazofikishwa mahakamani zina ushahidi na zimefanyiwa utafiti wa kina ili kuwezesha utoaji haki.

Jaji De Mello ambaye pia ni Jaji wa Mahakama Kuu, aliyasema hayo juzi wakati wa akifungua mkutano wa wadau wa haki jinai ulioandaliwa Shirika la Jukwaa la Utu wa Mtoto kwa kushirikiana na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA).

" Utoaji haki ni lazima ushahidi unaotolewa usiache shaka hata kidogo na Tanzania tunafuata sheria za Jumuiya ya Madola ambao kukiwa na shaka kidogo inatolewa mahakamani," alisema.

Aliwataka wadau wa mashauri wakiwamo wapelelezi kufanya utafiti na uchunguzi wa kina na kuwa na mashahidi ambao watatoa ushahidi usio na shaka ili kuwezesha utoaji haki kwa mashauri hayo.

Naye Mwanabaraka Mnyukwa wa IJA, alisema chuo kimekuwa kikitoa mafunzo kwa wadau kama majaji, mahakimu, mawakili wa Serikali na wa kujitegemea ili kushughulikia mashauri ya watoto wakiwamo wahanga wa ukatili wa kingono.

Kwa upande wa Mkurugenzi Mtendaji wa CDF, Koshuma Mtengeti, alisema mkutano wa wadau umeandaliwa ili kutafakari na kuja na mikakati ya pamoja ya kuimarisha upelelezi, uratibu wa wapelelezi, uendeshaji wa mashtaka na kupatikana kwa haki kwa watoto waliopitia ukatili wa kingono.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni mama ya Bank of Africa, Amine Bouabid (kulia), akimkabidhi tuzo Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni za Super Group of companies, Seif Seif (katikati), kutokana na kampuni hiyo kuwa mmoja wa wateja wakubwa wa benki katika kipindi cha miaka 25, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Afrika (BOA) Tanzania, Adamu Mihayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Simiyu ilivyojipanga kupunguza udumavu, ukondefu wa watoto

**Na Happy Severine,** BARIADI

MKOA wa Simiyu umesema umejipanga kupunguza asilimia ya watoto chini ya miaka 5 wenye udumavu kutoka asilimia 31.2 ya mwaka 2020 na kufikia asilimia 15.6.

Kadhalika, umesema umejipanga kupunguza ukondefu kutoka asilimia 4.6 hadi 2.3 kufikia mwaka 2025.

Hayo yalielezwa na Ofisa lishe mkoa wa Simiyu, Chacha Magige, alipozungumza na mwandishi wa habari na kueleza kuwa mkoa umeweka mikakati madhubuti ya kupunguza ukomavu na udumavu kwa kipindi cha miaka mitano.

Magige alisema kuwa kwa sasa mkoa una tatizo la udumavu kwa asilimia 31.2 na ukondefu asilimia 15.6 na ndiyo sababu ya kuongeza uwekezaji katika kutoa elimu ya masuala ya lishe na ulishaji wa watoto wachanga na wadogo chini ya miaka miwili, unaotolewa na vituo vya kutolea huduma za afya kwa asilimia 91.0 kwa mwaka 2020 ili kufikia asilimia 100 mwaka 2025.

Alisema kuwa mbali na uwekezaji wa elimu kwa jamii, pia watawajengea uwezo wataalam wa afya kwa ajili ya kutoa huduma za lishe katika ngazi za mikoa, halmashauri pamoja na vituo vya kutolea huduma za afya.

Costantine Mathia mkazi wa mji wa Bariadi, alisema udumavu na ukondefu kwa Mkoa wa Simiyu ni mwiba kwa sababu wakazi wengi hawajui na kuzingatia lishe bora na namna ya ulishaji wa watoto wadogo.

Alisema mbali na wakazi hao kulima vyakula mbalimbali, bado elimu inahitajika sana hasa maeneo ya vijijini kuhusu suala la lishe bora kwao na watoto wao.

Elimu juu ya lishe inahitajika sana... wakazi wengi wa Mkoa wa Simiyu hawajawa makini au hawaelewi ni vyakula vipi na wakati gani na kwa mchanganyiko upi unafaa kwa afya za watoto wao," alisema.

Agripina Lusekya, mhudumu wa afya katika Kituo cha afya Muungano, alisema suala la lishe kwa wakazi wa mji wa bariadi bado ni changamoto mbali na kuwaelimisha kila siku wajawazito na kinamama wanyonyeshao kuhusu vyakula vipi vya lishe lakini bado tatizo lipo.

Lusehekya alishauri elimu iendelee kutolewa ili ndani ya miaka mitano ya malengo ya mkoa yaweze kutimia na kuondoa ama kupunguza kabisa tatizo la udumavu na ukomavu.

Baadhi ya kinamama wanyonyeshao wa halmashauri ya mjili bado elimu inahitajika na kuomba uongozi wa vituo vya afya na zahanati zenye huduma ya mama na motto waendelee kuwaelimisha na kuwauzia unga lishe wa watoto wao pamoja na kuwainishia vyakula sahihi vya watoto wao.

# Wazazi washauriwa matibabu ya watoto wenye kichwa kikubwa

**Na Sabato Kasika**

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, amewataka wakazi wa mkoa huo walio na watoto wenye ulemavu wa kichwa kikubwa na mgongo wazi kujitokeza, ili watoto wao wapimwe afya.

Dk. Mfaume alitoa wito huo jijini Dar es Salaam alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Watoto Wenye Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi ambayo yanaanza leo. Maadhimisho hayo kitaifa yanafanyika jijini Dar es Salaam na yataanza leo ambapo madaktari watachunguza afya za watoto wenye ulemavu huo kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja na kutoa ushauri.

"Dar es Salaam kuna zaidi ya watoto 700 wenye ulemavu huo, hivyo wito wangu kwa wazazi na walezi ni kwamba, wajitokeze kwa wingi katika viwanja vya Mnazi Mmoja ili watoto wao wapime afya," alisema Dk. Mfaume.

Alisema kumekuwapo na taarifa kuwa baadhi ya wazazi na walezi wanawaficha watoto, kwa imani kuwa wamelogwa au ni mkosi na kusisitiza kuwa hayana ukweli badala yake wajitokeze, ili watoto wahudumiwe.

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija, ambaye maadhimisho hayo yanafanyika kwenye wilaya yake, alisema, hiyo fursa kwa wakazi wa Ilala wenye watoto walio na ulemavu huo kujitokeza kwa wingi.

"Kama madaktari wameamua kutoa huduma za afya bure kwa ajili ya watoto wenye ulemavu huo, hiyo si fursa ya kukosa, hivyo nami niwahimize kila mzazi au mlezi mwenye mtoto wa ulemavu huo ajitokeze," alisema Ludigija.

Mratibu wa Chama cha Wazazi Wenye Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi Tanzania (ASB AHT), Hidaya Alawi, alisema maadhimisho hayo yatafikia kilele chake Oktoba 25, mwaka huu.

"Katika maadhimisho haya, tumeshirikisha madaktari bingwa wakiwamo kutoka Taasisi ya Mifupa (MOI) watakaopima afya za watoto 500 wenye ulemavu huo, ambao hawajawahi kupimwa," alisema Hidaya.

Hidaya alisema, Jumapili kutakuwa na matembezi ya hisani kuanzia MOI hadi viwanja vya Mnazi Mmoja, yakiongozwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu.

"Lengo la matembezi hayo ni kuchangisha Sh. milioni 360 ambazo zitatumika kwa ajili ya kulipia gharama za matibabu kwa watoto wenye ulemavu huo ambao wamelazwa katika hospitali mbalimbali nchini," alisema.

Mratibu huyo alifafanua kuwa Oktoba 25 ambayo itakuwa ni kilele cha maadhimisho hayo, kutakuwa na kongamano za kujadili kwa kina athari za ugonjwa huo kuanzia kwa watoto, familia na jamii kwa ujumla. "Kwa ujumla ni kwamba, kuanzia Ijumaa kutakuwa na shughuli mbalimbali zinazoendelea kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja, kwani mbali na watoto kupimwa, kutakuwapo na chanjo ya UVIKO-19," alisema.



Ofisa Msimamizi wa Kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Godfrey Kumwembe akiwaelimisha wafanyabiashara kuhusu umuhimu wa kulipa kodi, wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi, wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma jana. **PICHA: TRA**

# DAS ahimiza kutoa, kudai risiti za EFD

**Na Mwandishi Wetu,**
TUNDURU

WAFANYABIASHARA wilayani Tunduru mkoani Ruvuma wamehimizwa kutoa risiti stahiki kila wanapouza bidhaa na huduma huku wananchi pia wakitakiwa kudai na kukagua risiti kila wanaponunua bidhaa.

Wito huo ulitolewa jana na Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Joshua John, alipozungumza na timu ya maofisa kutoka Mamlaka ya Mapato (TRA) Makao Makuu Dar es Salaam walipowasili wilayani humo kwa ajili ya kufanya kampeni ya elimu kwa mlipakodi mlango kwa mlango.

"Ninatoa wito kwa wafanyabiashara wenye mashine za EFD kuhakikisha wanatoa risiti stahiki kila baada ya kufanya mauzo na wanunuzi wadai risiti na kuzikagua kama kiasi kilichoandikwa kinafanana na fedha waliyonunulia bidhaa.Hii itasaidia kuongeza mapato ya serikali kwa maendeleo ya taifa letu," alisema.

Ofisa Msimamizi wa Kodi wa TRA, Mkoa wa Ruvuma, Justine Katiti, alielezea maendeleo ya kampeni hiyo tangu kuanza kwake Oktoba 13, mwaka huu mkoani humo, akibainisha kuwa mpaka sasa maofisa hao wameshawafikia walipakodi takribani 1,000 katika wilaya za Songea, Mbinga na Nyasa.

"Kwa sasa tupo hapa wilayani Mbinga na tukimaliza tutaelekea Wilaya za Namtumbo na Madaba," alisema Katiti.

Aliongeza kuwa katika kampeni hiyo, pamoja na mambo mengine, wafanyabiashara wamepewa elimu ya matumizi sahihi ya mashine za EFD.

"Tumefanikiwa kuwaelimisha masuala mbalimbali ya kodi ikiwapo matumizi sahihi ya mashine za EFD na kuwakumbusha kwamba kutokutoa risiti ni kosa kwa mujibu wa sheria na adhabu yake ni kati ya Sh. milioni 3 hadi 4.5 kwa mfanyabiashara atakayebainika hatoi risiti," alisema.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wafanyabiashara wa wilaya hiyo walisema kuwa wamefurahishwa na elimu iliyotolewa na maofisa hao wa TRA.

"Leo nimefurahi kutembelewa na maofisa wa TRA ambapo wamenifundisha kuwa makini na matapeli wanaojifanya watumishi wa TRA na wamenikumbusha kutoa risiti za EFD kila ninapofanya mauzo," alisema Esau Pera, mfanyabiashara wa pembejeo za kilimo.

Rashid Mambulu ni mfanyabiashara wa vifaa vya umeme wilayani humo ambapo aliwaomba wafanyabiashara wenzake kuzingatia utoaji wa risiti sahihi kwa wateja wao ili kuepukana na adhabu ya kutokutoa risiti za EFD.

"Kati ya mambo mengi niliyofundishwa na maofisa wetu wa TRA ni pamoja na kunikumbusha kukata risiti sahihi za EFD na wameniambia adhabu ya kutokutoa risiti ni Sh. milioni tatu hadi 4.5, hivyo ninawaomba wafanyabiashara wenzangu tuzingatie utoaji wa risiti sahihi ili tuepukane na faini za kutokutoa risiti," alisema.

Timu ya maofisa wanaofanya kampeni ya elimu kwa mlipakodi mkoani Ruvuma iko wilayani Tunduru ikiendelea kutoa elimu ya kodi na baada ya wilaya hiyo wataelekea Wilaya za Namtumbo na Madaba.

## Mkandarasi apewa siku 7 ujenzi daraja

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MBOZI

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, amempa siku saba Meneja wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) Wilaya ya Mbozi, Mhandisi Naftari Chaula, kuhakikisha daraja linalounganisha vijiji vya Idiwili na Ilomba kwenye mto Songwe linakamilika na kuanza kutumika.

Alitoa agizo hilo jana baada ya kukagua daraja hilo na kupokea malalamiko ya wananchi juu ya kusuasua kwa ujenzi wake, ikiwa ni siku ya kwanza ya ziara yake ya siku nne ya kukagua shughuli za maendeleo katika Wilaya ya Mbozi.

Alisema mkandarasi wa mradi huo, ambaye ni kampuni ya Lumo kutoka jijini Dar es salaam tayari alishalipwa fedha zote kwa mujibu wa mkataba, hivyo kitendo cha mradi huo kushindwa kukamilika kwa wakati serikali ni uzembe ambao hauvumiliki.

"Natoa ahadi kama kiongozi Mkuu wa Mkoa huu hatukuja hapa kufanya sanaa au kiini macho hapa na ndani ya siku saba kama daraja hili halijakamilika nimemwambia injinia hapa atafute kazi nyingine," alisema.

Mgumba alisema kwa mujibu wa mkataba huyo alitakiwa kumaliza kazi ya ujenzi wa daraja hilo mwezi Januari mwaka huu lakini aliomba nyongeza ya muda hadi Septemba 30, mwaka huu.


"Wananchi naomba muwe na imani na serikali yenu maana hatukuja kubembelezana hapa kwa kuwa mkandarasi alishapewa fedha zote na muda wa nyongeza alioomba ili amalizie kazi umeisha" , alisisitiza Mgumba.

Awali kabla ya Mkuu wa Mkoa kutoa agizo hilo, mmoja wa wananchi wa Kijiji cha Ilomba, Jumamosi Shikombo, akiuliza swali alitaka kujua sababu zinazosababisha ujenzi wa daraja hilo kusuasua na kusababisha adhan kwa wananchi kuhatarisha maisha yao kwa kupita kwenye kivuko kilichojengwa kienyeji.

Alisema kivuko kinachotumika kwa sasa ni hatari kwa usalama wa watumiaji hususani kipindi hiki amabacho mvua za msimu zinztarajia kuanza kunyesha.

Naye Mhandisi Chaula alisema muda uliotolewa na Mkuu wa Mkoa unatosha kukamilisha mradi huo.

Aidha, Mhandisi Chaula alisema mbali na daraja hilo, serikali imetenga Sh. milioni 134 kwa ajili ya kuiimarisha barabara hiyo ya Idiwili -Ilomba yenye urefu wa kilometa saba kwa kujenga kwa kiwango cha changalawe.




Ukurasa 13

Tufikirieni saa za baa penye kodi, ajira zaidi



## Ngozi ya mnyama; utajiri ambao wengi hawajazinduka kutambua thamani yake

Ukurasa 12

BUFE
IJUMAA OKTOBA 22, 2021
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

MATUNDA YA WORLD VISION…

# Mwenye ulemavu, fundi tangu 1978 aunganisha na kilimo kuona mageuzi

## • Kutoka kutegemea, hadi kutegemewa

**Na Renatha Msungu, CHEMBA**

NI kama hadithi, lakini uhalisia ndio huo ni mwanamke mwenye umri wa miaka 60, mwenye ulemavu wa miguu anayejishughulisha na kilimo cha kisasa, huku cherehani anayotumia kushona katika makazi yake, eneo la Kwamtoro, wilayani Chemba, Dodoma.

Grace Andrea ni mama wa wajukuu wawili wa kike walioko shule ya sekondari, akiwatunza kupitia kazi hiyo ya kilimo cha kisasa, baada ya kupata mafunzo na mbegu bora kutoka Shirika la World Vision.

Leo yamemuwezesha hivi sasa kupata mazao mengi katika eneo la ekari chache anazolipa tofauti na ilivyokuwa mwanzo, alikuwa akipata mazao kidogo kwa kutotumia Kilimo cha kisasa.

World Vision, shirika lililojikita katika kusaidia watu wa hali ya chini kupitia miradi mbalimbali, inayoendesha pia wanamradi wa boresha afya ya mama na motto, ambao nao huwasaidia wakinamama wengi kuwapa elimu katika suala hilo.

Mama huyo amekuwa mfano wa kuigwa katika kijiji hicho, kutokana na kuwa ameepuka kuwa ombaomba kutokana na ulemavu aliyokuwa nao na badala yake amekuwa wa kujitegemea, ikiwamo kuwasaidia walemavu wengine wenye hali kama yake katika kuwa elimu.

**MSAADA WORLD**

Ni shirika lililopo katika mikoa mbalimbali hapa nchini, ikiwamo Dodoma, ikiendesha mafunzo ya kila mara kwa jamii, kuhakikisha wanainuka kiuchumi, ikiwamo kilimo na biashara, hasa vijijini.

Grace Andrea ni mwenye ulemavu, mnufaika anayesema matokeo chanya ya mafunzo ya kilimo yatolewayo, ndio imezaa matunda hayo.

Anafafanua kuwa, kupitia kilimo ambacho anafanya, sasa anasomesha wajukuu zake na kuendesha maisha ya familia inayomtegemea kimaisha.

Grace anaiwekea shukrani muwezeshaji wake, asasi ya World Vision, ambayo imekuwa ikimtembelea kila anapoiita kujua maendeleo yake katika kilimo na ushonaji anaoufanya, kuhakikisha anasonga mbele katika maisha.

Anasema, aliamua kufanya hivyo, ili kuepuka kukimbiwa na jamii kutokana na kuamini mtu akiwa mlemavu basi hawezi kufanya kazi yoyote jambo ambalo sio kweli ni dhana potofu, ambayo wanadamu wamejiwekea.

Anasema, kutokana na hilo aliamua kufanya shughuli zake zinazomuinua kiuchumi yeye na familia yake, mahsusi kilimo na ushonaji nguo za wanawake na watoto, kwake kwa mtoto.

**ALIPOANZIA USHONAJI**

Grace anasimulia, alianza mwaka 1978, akiwa binti mdogo na mpaka akafanikiwa kupata familia yake na kuendela na ushonaji hadi sasa, pamoja na hali aliyo nayo.



Grace Andrea akizungumza na mwanahabari.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

Anasema anapata wateja, japo sio wengi sana kama ilivyokuwa awali, lakini akifurahia amewafundisha walemavu wengine, ambao nao hivi sasa wanashona na wanajiinua kiuchumi.

Anafafanua kuwa anatumia cherehani ya mkono kwa sababu ni mlemavu miguu, hivyo anashona mitindo mbalimbali ya kike, ambayo wateja wengi humfuata kutokana na uaminifu aliokuwa nao katika ushonaji.

Grace anajivunia mafanikio, sasa anasomesha wajukuu na kulisha familia yake.

**KUTOKA WORLD VISION**

Joseph Kilimba, ni msimamizi wa miradi inayowainua kinamama kiuchumi, anasema shirika hilo limekuwa likiwapatia mafunzo ya kilimo, ikiwamo kuwapa mbegu bora kinamama na jamii kwa ujumla, kuwapa tija.

Hivi sasa kuna kinamama wengi ambao wameunda vikundi vya vikoba kupitia kilimo wakiwa na mafamikio na World Vision, wamekuwa wakiwapita kila mara kuviangalia

Anasema, wanafurahi kuona kinamama hao hawabaki nyuma, japo wapo ambao wamekuwa wazito kuhudhuria mafunzo ambayo ni muhimu sana kwao, katika kuendeleza familia zao.

Kilimba anasema, pia wanawafundisha kutengeneza lishe bora, ambacho wanatengeneza na kuwauzia wengine, ili kuhakikisha afya za watoto wao zinakuwa bora.

Anafafanua kuwa, lengo lao ni kuona kinamama wanapata mafunzo kutoka World Vision na kupiga hatua, wakawa mfano wa kuigwa kimaisha, huku wakiwa na kipato cha kuwainua kiuchumi wasiaki nyuma.

Kutokana na hilo aliwataka kinamama na jamii kwa ujumla kutobweteka na badala yake wajifunze kuhakikisha wanasonga mbele.

Anasema vikundi vingi vya wanawake vina uhai, kwa sababu ya kuzingatia mafunzo mbalimbali wanayopewa na World Vision, kupitia wataalam wao ambao wamewaweka katika vijiji mbalimbali, ili kuhakikisha jamii inapata mafunzo ya kuinuana wenyewe na wanasonga mbele, badala ya kuwa tegemezi, jambo ambalo halikubaliki.

BIASHARA

# Ngozi ya mnyama; utajiri ambao wengi hawajazinduka kutambua thamani yake

- Hatari: Kumchapa, kumwekea muhuri na kutomsafisha
- Panakimbiliwa nyama, maziwa kidogo, 'ngozi ya kulalia'
- Longido sasa mambo moto, wadau mifugo na jambo lao

**Na Zanura Mollel, LONGIDO.**

TANZANIA ni nchi ya pili barani Afrika kwa wingi wa ng'ombe baada ya Ethiopia na Sudan. Zaidi ya asilimia 90 ya mifugo iliyopo nchini ni ya asili, wanyama wanaosadikika wamezoea mazingira magumu na wanastahimili hali hiyo.

Je, utajiri huo unaifaidishaje jamii nchini? Taswira ya majibu inaanzia namna uzalishaji huo wa mifugo umegawanyika katika mifumo miwili; huria na shadidi, unaotiliwa mkazo nchini, kwani inatajwa kupanuka sokoni.

Ufugaji huria unafanywa na wanaohama. Ni mfumo unaotegemea malisho na maji kwa msimu na matokeo yake, wafugaji wanahama, wahusika wake wanajumuisha jamii ya Wamasai.

Hadi sasa, ufugaji huria unatajwa kuwa n

a matatizo ya utunzaji duni wa mifugo, teknolojia ya chini kuhodhi mifugo mingi zaidi ya uwezo wa ardhi na ukosefu wa soko bora, lakini mfumo huo bado unategemewa kwa miaka mingi sana.



Ng'ombe wakiwa sokoni wilayani Longido.

### MAZAO MIFUGO

Kwenye mifugo kuna mazao yanayopatikana zikiwamo ngozi na maziwa. Ila wafugaji huthamini nyama na kuiacha uzito mdogo, lakini mazao ngozi na maziwa hayana uzito mkubwa hasa sokoni.

Gazeti la Nipashe limefanya tafiti kushirikiana na wadau wa mifugo, kupata undani wa mnyororo wa thamani wa zao la ngozi kwa wafugaji nchini.

### ZAO LA NGOZI.

Je, ngozi ni nini? Hilo ni ganda la nje linalofunika mwili wa mnyama, binadamu au kiumbe chochote.

Kitaalamu ngozi ya wanyama imegawanyika mara mbili. Kuna ngozi za wanyama wakubwa kama vile farasi, ngamia, ng'ombe na nyati na aina nyingine ni za wanyama wadogo kama mbuzi, kondoo na sungura.

Hivyo, ngozi inayochunwa ina matabaka, matatu; la nje (epidermis) ambayo kuna la nje inayokua kila mara. Kwa upande wa nje hukauka na kusinyaa, kwa wanyama wengi wakionekana na vinyweleo na manyoya.

Tabaka la kati la ngozi liko nene na muhimu kuliko matabaka mengine ya ngozi. Asilimia 85 ya ngozi hiyo inatajwa kutumika kutoa ngozi inayoandaliwa kutengenezea bidhaa mbalimbali kama vile viatu, mikanda, makoti, mikoba, mabegi na gundi.

Tabaka hilo lina sehemu kuu mbili. Pale mnyama anapokuwa hai hufanya kazi ya kurekebisha joto la mwili.

Wataalamu wanafafanua, unene sehemu ya ndani ni mara tatu ya nje. Uwiano wa sehemu hizo mbili, hutofautiana kulingana na umri na aina ya mnyama.

### UMUHIMU WAKE

Wataalamu na wadau sokoni, wanafananisha ngozi ni malighafi ya thamani katika kuitengeneza bidhaa kama nguo, begi, pochi,viatu na mikoba.

Pia, wanaitaja kutumika katika tiba, mfano hai ni ngozi ya nguruwe inatumika kufunika vidonda vitokanavyo na kuungua moto au michubuko, hali kadhalika kurekebisha majeraha sehemu ambako ngozi imetoka.

### RAI YA MDAU

Mkufunzi Mkuu wa Wakala wa Mafunzo ya Mifugo kutoka Taasisi ya Tengeru - Arusha, Frank Mosha, anasema thamani ya zao ngozi inayopatokana kwa wingi wilayani Longido, inatoa nyuzi za kushonea vidonda au majeraha na mahitaji ya kufanana nayo.

Ili kupata ngozi bora wafugaji nchini, anashauri kuzingatia njia bora za kuzalisha mifugo yenye ngozi imara kwa kuangalia aina na koo za mifugo. Upana wa ngozi, pia unazingatiwa aina.

Mtaalamu Mosha anasema, wanyama wenye nundu, ngozi yao hukatwa vipande viwili badala ya kubaki kipande kimoja. Hivyo, aina ya ng'ombe inatafsiri aina ya ngozi.

Kuna umri wa kuchinja mifugo. Mnyama akichinjwa na umri mdogo kuanzia umri miaka mitatu hadi mitano kwa ng'ombe na miwili hadi mitatu kwa mbuzi na kondoo hutoa ngozi nyororo na yenye ujazo wa nyuzi za protini,

Mosha anasisitiza kwamba, mnyama anapokuwa na umri mkubwa na hakutunzwa vizuri, anakabiliwa na matatizo mbalimbali yanayoweza kuathiri ubora wa ngozi yake.

Kuna hadhari anayotoa kwamba, kupiga chapa ngozi ya mifugo bila ya kuzingatia ubora na sehemu muhimu, imapaswa kuwa katika mbadala kama vile gotini, kwenye nundu na shavuni.

Pia, anasema wafugaji wengi hutumia chapa ya moto kutambulisha mifugo yao, zinazopigwa sehemu kama mbavuni na shingoni, hata kuharibu ngozi kwa jumla.

Chapa ya moto huharibu tabaka la nje na kati ambalo ni muhimu katika kupata ngozi bora na za aina hiyo, hukosa uimara makovu yanashindwa kupenyeza kemikali wakati wa usindikaji na kushusha ubora wake.

Lingine inatajwa mfugaji anaposhindwa kudhibiti magonjwa ya mifugo na kuua vidudu vya nje kama kupe na chawa, kwa kuwaogesha, walau mara mbili kwa wiki, ina athari yake kwenye ngozi.

Mosha anasema baadhi ya magonjwa yatokanayo na athari hizo ni; upele wa ngozi, pia wa ndui; mapunye; na kimeta. Mifugo iliyopata madhara ya magonjwa, daima haiwezi kuwa na ngozi bora kwa matumizi ya viwandani.

Daima haishauriwi mifugo kupata mikwaruzo itakonayo na miba, pembe, fimbo na nyaya za uzio zenye ncha kali kwani inasababisha kuwapo makovu katika tabaka la nje na kati, ambazo ni muhimu kupata ngozi bora iliyosindikwa.

### WADAU MIFUGO.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Mazao ya mifugo, Usalama wa Chakula na Lishe, katika Wizara ya Mifugo, Gabriel Bura, ameiambia Nipashe kwamba, katika upatikanaji masoko ya uhakika kununua ngozi, serikali imewezesha Longido kuwa na viwanda vya kushughulikia malighafi hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti wa Sera na Kuondoa Umasikini nchini (REPOA) Dk. Donald Mmari, anasema kunahitajika ushindani kwenye zao la ngozi nchini.

Mtafiti na mtaalamu wa ngozi, kutoka Shirika la Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), Dk. Cecilia China, anasema asasi yao ilianzishwa mwaka 1979 kusaidia viwanda kupata malighafi inayopatikana nchini, kuziwezesha kuzalisha kiushindani na kuwa endelevu kupitia taifa.

Anasema jumla ya wiwanda vya ngozi sita na viwanda vya bidhaa za ngozi 29, vimeshapatiwa mafunzo ya kuongeza mnyororo wa thamani kupitia bidhaa ngozi mwezi machi mwaka huu na matokeo yanayotarajiwa ni kuongezeka ubora wa ngozi na bidhaa zake, ili kukidhi vigezo vya soko la ndani na kimataifa.

### MFUGAJI WA LONGIDO

Katika hoja hiyo, mkazi kutoka jamii ya wafugaji walioko Longido, Kasaine Lemaiba, anasema mifugo mingi ya jamii ya kimasai,. inapigwa chapa kulingana nauko ulivyo, anatetea kuwa ndio utambulisho wa mifugo yao inapopotea wawapo malishoni.

Anafafanua peye mauzo, ngozi za wanyama wakubwa kama ng'ombe wanatumia kama matandiko ya kulalia, huku wanyama wadogo kama mbuzi na kondoo wanawauzia wateja kutoka nchi jirani ya Kenya.

Katika kupambana na uharibufu wa zao la ngozi, wameweka mpango mkakati wa kukutana na wazee wa mila na kuangalia namna watakavyoboresha mifugo katika upigaji wao wa chapa.

Kuhusu malisho ya kutosha, mfugaji huyo na kiongozi wa ukoo anasema, kuna mimea vamizi kutoka nyanda za malisho, hata imewapotezea majani, jambo lililowasukuma kwenye ufugaji wa kuhama, kusaka malisho.

Pia, anataja maeneo ya malisho yanapungua kutokana na serikali kutenga maeneo makubwa kwa ajili ya shughuli za uhifadhi na utalii, akilalamika wafugaji wamesahaulika.

### SERA NA SHERIA

Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006, inanagalia katika uongezaji mapato ya wafugaji, kujitosheleza kwa uzalishaji chakula cha asili ya wanyama na kukuza mchango wake katika pato la taifa.

Sera inaangalia udhibiti wa kuingiza mifugo kutoka nje ya nchi kushindana na soko la nchini, vilevile ikiguisa usajili wa wanyama na ufuatiliaji wake, maarifa asilia ya kiufundi, magonjwa yanayoibuka, bidhaa za mifugo, taasisi za udhibiti na mifumo ya maabara ya mifugo.

Pia, penye angalizo la Sheria ya Biashara ta Ngozi ya Mwaka 2008, inazingatia ukuzaji, kudhibiti uzalishaji na uhifadhi wa ngozi, kukiendelea kukuza biashara kupitia ukaguzi wa kila mara, kuboresha ngozi na bidhaa zake, ili kukidhi masoko ya ndani na kimatifa.


Sheria inalenga kuhakikisha uzalishaji unafanyika kwa njia rafiki wa mazingira shirikishi kwa jamii. Sheria iimeunda kamati ya ushauri ya ngozi na bidhaa zake katika kila halmashauri na kijiji, kushauri na kutekeleza sheria hiyo kwa ufanisi.



Bidhaa ngozi ikiwa katika hatua za maandalizi, mjini Sumbawanga. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Tufikirieni saa za baa penye kodi, ajira zaidi







**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

NASIKIA pombe hata kwenye baadhi ya maandiko ya kiimani inatamkwa. Sijasoma eneo hilo, kwa sababu nizijuazo mimi na sitataka niulizwe zipi na kwanini. Ila sijasoma, mliosoma hapo niungeni mkono kama ni kweli.

Kama basi ndiyo hivyo, najua pombe hulevya na ikilevya tarajia chochote kwa mlevi. Anaweza kuwa mpole sana au mkali. Pia, anaweza kuwa kama zezeta akijichekesha. Hiyo ni pombe!

Wapo wanaoamini kuwa humpotezea mtu usongo wa mawazo na kuwa mpya wakati amelewa, lakini wapo wanaosema huwa inaahirisha tu matatizo na huenda ikiisha kichwani yakawa maradufu.

Kuna wakati tunashuhudia watu kuzuiwa kunywa pombe mapema, kwa mtazamo au angalizo wanaweza wasiende kazini, au wakienda wakashindwa kuzalisha kama inavyotarajiwa. Hivvyo, kuwekwa muda maalumu wa kunywa pombe.

Ni kwamba, pombe zina muda maalumu, lakini migahawa ya chakula haina muda maalumu. Unajiuliza ni sababu gani? Mbona kuna wakati huwa tunaambiwa kuwa shibe ni mwana malevya? Kumbe ukishiba sana unalewa!

Nchini tulishawahi kuagizwa baa zote zisifunguliwe kabla ya saa 10 jioni, hususan siku za kazi na kufungwa saa tano usiku.

Hapo Braza Korona hakuwa ameshatutembelea, lakini ikawa hivyo na kwamba hata michezo ile ya kusokomeza mezani (Pool Table) nayo hapana!

Alipowasili Braza Korona wala hatukusikia fungueni baa saa fulani, fungeni saa fulani. Hakukuwa na haja, kwa sababu baa zilishajifunga zenyewe tu kwa amri ya awali.

Ni wakati wenye baa wakafanya kazi katika mazingira na wakati mgumu, wakakosa wateja, wakapunguza watumishi ambao waliingia mitaani kufanya ajira zingine, huenda baadhi ambazo si sahihi zinapishana na sheria.

Wenye hizo baa wakakosa fedha za kuwalipa mishahara, sasa kwanini wasipunguze mzigo? Wakashindwa hata kulipia gharama za kujiendesha, kwa kodi za pango, umeme na maji! Baa zingine zikageuka nyumba za ibada na baadhi shule za chekechea.

Braza Korona alipozuru kwa majirani zetu Kenya, wao ikawa mbaya zaidi wakaambiwa baa zifunguliwe saa 11 jioni na kufungwa saa mbili usiku. Hebu niambie, kunafanyika biashara au kijiwe?

Lakini, angalau hao walikuwa na sababu za Braza Korona. Sisi je? Huwa kuna hulka nyingine za watu hadi wakinywa ndio wanachapa kazi.

Kuna simulizi bingwa wa tiba aliyekuwa na jina linafanana na madini hivi, alikuwa hapasui mpaka agide. Sasa huyo amgezuia subuhi, jamani inakuwaje?

Kuna maswali ambayo hujitokeza katika sura mpya ya shilingi kwenye hatima ya soda, nyamachoma na chipsi, ambazo ni vipi zinazaa matokeo kwenye kodi, sambamba na ajira?

Ajira zikikosekana, huwa na athari zake, vibaka na majambazi mitaani? Mimi mstaafu nimejikalia nyumbani sina la kufanya, nina mafao yangu nimesotea nataka niende kukaa na wastaafu wenzangu pabu asubuhi, naambiwa saa hiyo imekatazwa.

Si mbaya, pia tuangalie namna gani mazingira hayo katika mustakabali wa mauzo yanayozaa fursa ya wateja, kipato cha kodi na kitengeneza fursa za ajira. Au Vipi? Alamsiki!

UCHUMI

## MAPYA YA TABASAMU;

# Serikali yaingiza Mil. 480/- ujenzi bwawa kijiji chenye nusu ng'ombe wilaya Liwale

## • Waziri Ulega awatembelea kuwapa neno

**Na Sabato Kasika**

BAADHI ya watu nchini wamekuwa wakifuga hasa ng'ombe, mbuzi na kondoo kwa mtindo wa kuhama kila mara kutoka mmoja kwenda mwingine kwa lengo la kutafutia mifugo yao maji na malisho.

Ni ufugaji wa aina hiyo umekuwa ukisababisha kutokea migogoro kati yao na wakulima na kuleta madhara kwa jamii, ikiwamo hatua ya mapigano na kudhuru watu, wanyama na mimea yenye thamani.

Wilaya ya Liwale mkoani Lindi ni miongoni mwa maeneo ambayo hayakuwa na mifugo mingi kihistoria, lakini kwa sasa tayari wafugaji wa ng'ombe wamehamia huko kwa ajili ya kutafuta malisho na maji.



Naibu Waziri, Abdallah Ulega akiwa kwenye mkutano wa hadhara, katika Kijiji cha Kimambi, kutakapojengwa bwawa la mifugo. Kulia kwake ni Mkuu wa Wilaya ya Liwale, Judith Nguli. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

Ni hali iliyoisukumu serikali kutenga Sh. milioni 480 kwa ajili ya kuchimba bwawa ambalo litakuwa maalum kwa ajili ya mifugo ya wafugaji, ambao wapo kwenye baadhi ya maeneo ya wilaya hiyo.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega anasema katika bajeti ya mwaka huu, serikali itajenga bwawa la kunyweshea mifugo lenye thamani hiyo ya fedha katika Kijiji cha Kimambi, wilayani humo.

Akiwa ziarani hivi karibuni kwa lengo la kusikiliza kero za wafugaji na wakulima, Ulega anasema bwawa hilo litasaidia kutatua shida ya maji ambayo inawakabili wafugaji wa maeneo hayo.

Naibu Waziri huyo, pia anawataka viongozi wa wilaya hiyo kuhakikisha kwamba pesa zitakapofikishwa kwao, zitumike kwa kazi husika ambayo ni ujenzi wa bwawa la kunyweshea mifugo.

Mbali na kutengwa kwa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya bwawa, Ulega anaongeza kuwa, vijiji vya Kimambi na Luwele, kila kimoja kitakuwa na majosho kwa ajili ya mifugo ya maeneo hayo.

### HALI YA MIFUGO

Ofisa Mifugo wa wilaya hiyo, Benarrd Kivamba, anasema Liwale ina jumla ya ng'ombe 30,689, mbuzi 11,797 na kondoo 2,462, na anafafanua kuwa Kijiji cha Kimambi ndicho kinachoongoza kwa kuwa na ng'ombe wengi wilayani humo.

"Yaani ni kwamba ng'ombe 14,000 kati ya hao 30,689 wapo katika kijiji cha Kimambi na ndiyo maana serikali inataka kujenga bwawa la kunywesha maji ng'ombe na mifugo mingine," anasema Kivamba.

Ofisa Mifugo huyo anasema, ofisi yake imekuwa ikijitahidi kuhakikisha wilaya hiyo haina migogoro kati ya wakulima na wafugaji kwa kushirikisha makundi hayo kila linapotaka kutokea jambo ambalo linaweza kusababisha uhasama.

"Kama yalivyo kwenye baadhi ya maeneo nchini ambayo yamepokea wafugaji, ndivyo kwa Liwale ilivyo, lakini tunajitahidi kuhakikisha hakuna migogoro kama ambayo tunasikia ikitokea kwingine," anasema.

Anasema, makundi hayo kila mmoja lina umuhimu katika kuchangia maendeleo ya wilaya hiyo na kwamba hadi sasa wilaya hiyo ina minada miwili ya ng'ombe, katika Kijiji cha Kimambi na Zinga.

Lugora Uporo, ni kiongozi wa wafugaji wilayani humo, anaishukuru serikali kutoa pesa za ujenzi wa bwawa na anaongeza kuwa hawatarajii kuwapo migogoro katika vijiji vilivyotengwa kwa ajili yao wilayani humo.

"Tutaendelea kushirikiana wote kama Watanzania ili kuhakikisha kwamba kila mmoja anaishi kwa amani na utulivu na kufanya shughuli zake za maendeleo ikiwamo kilimo na ufugaji," anasema Uporo.

Katika hilo, Naibu Waziri anawataka viongozi wa serikali kuanzia ngazi za vitongoji, vijiji, kata hadi wilaya kuhakikisha wanaunda kamati za maridhiano kwa ajili ya kusuluhisha migogoro ya wakulima na wafugaji inapojitokeza.

Ulega anasema, kamati za maridhiano zina mchango mkubwa katika kusaidia kumaliza tofauti kati ya makundi hayo mawili na kwamba amekuwa akitoa maelekezo kwenye maeneo yote ya migogoro.

"Wakulima wamekuwa wakilalamikia wafugaji katika maeneo mbalimbali nchini kwa kusababishia matatizo ikiwamo kuharibiwa kwa mazao yao, hivyo kamati za maridhiano zinaweza kuleta suluhu," anasema.

Ulega anasema, kuwapo kwa kamati hizo kila eneo nchini, kunaweza kusaidia kushughulika na migogoro kati ya wakulima na wafugaji mapema kabla haijakuwa mikubwa na kuleta madhara.

Waziri pia anakemea vitendo vya baadhi ya wakulima na wafugaji kujichukulia sheria mkononi kwa kushambuliana kwa kuwa vinachangia kuwapo kwa uvunjifu wa amani miongoni mwao.

### ANGALIZO LA DC

Mkuu wa Wilaya ya Liwale, Judith Nguli, katika hilo anawataka wakulima na wafugaji kuendelea kuimarisha amani na utulivu miongoni mwao wakati serikali ikiweka mikakati ya kuhakikisha.

Mkuu wa Wilaya anawataka viongozi wa wafugaji kufuata sheria na utaratibu uliowekwa ikiwamo kuzingatia maeneo yaliyotengwa kwa ajili ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima kati yao na wakulima.

"Mtindo wa wafugaji kuhama katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili yenu na kwenda kuishi maeneo ambayo hamjatengewa, unaweza kusababisha migogoro kati yenu na wakulima," anasema Judith.

Pia, anawataka viongozi wa vijiji vilivyoruhusu wafugaji kutotoa vibali kwa wafugaji wapya, badala yake kama kuna shida katika maeneo yao, basi wazishughulikie na kuzipatia ufumbuzi.

"Kinachotakiwa nyie viongozi wa vijijini ni kuangalia kama kuna changamoto miongoni mwa wakulima na wafugaji katika maeneo yenu na kuzitafutia ufumbuzi ili makundi yote yaendelee kuishi kwa amani," anaeleza.



Ng'ombe wakiwa machungani, wilayani Liwale.



## Askofu wa Anglikana ataka hadhari corona

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Anglikana Tanzania Dayosisi ya Central Tanganyika, Dk. Dikson Chilongani, ameitaka jamii kuendelea kuchukua tahadhari ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa UVIKO-19.

Aidhaa Dk. Chilongani amesema kuwa bado ugonjwa upo na unaua, hivyo ni jukumu la kila Mtanzania kuchukua hatua ya kujikinga kwa kuwa umekuwa ukipoteza watu na nguvu kazi ya taifa.

Askofu huyo alisema hayo jijini Dodoma wakati akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kuzindua huduma ya Injili ya Kishindo.

Alisema kuwa hakuna sababu yoyote ya kupuuzia ugonjwa huo kwa kuwa bado upo na unaleta madhara makubwa na kupoteza nguvu kazi ndani ya taifa.

Akizungumza kuhusu uzinduzi huo wa Injili ya Kishondo, alisema kuwa lengo ni kupeleka injili kwenye jamii ya watu wote ikiwa ni sehemu ya kufikisha neno la Mungu ili wale wote ambao bado wanaendelea na vitendo viovu waachane navyo.

Askofu huyo amesema bado Watanzania wanatakiwa kuhubiriwa ili kuendelea kuyatenda matendo mema ambayo yatalifanya taifa kuwa katika hali ya utulivu na amani.

"Dayosisi ya Central Tanganyika imeanzisha huduma ya Injili ya Kishindo kwa lengo la kuifikia jamii kwa kuwajenga kiroho na kimwili.

"Lengo kubwa ni kuhakikisha vijana waliopo makanisani wanatoka na kufanya huduma ikiwa ni pamoja na kuibua vipaji vyao," alisema Dk. Chilongani.

Mkurugenzi wa Uinjilisti Dayosisi ya Central Tanganyika Mchungaji Canoni Prof. Grece Mbise alisema kuwa huduma ya uinjilisti wa Kishindo ni huduma ambayo inalenga kuwafanya vijana, wachungaji na wainjilisti kutoka na kuanza kuhubiri neno la Mungu.

"Huduma hii ni endelevu, na tumekuwa tukitoa mafunzo kwa wainjilisti na vijana kwa kuwajengea uwezo wa ujasili wa kuhubiri neno la Mungu kwa nia ya kuwafanya watu kumrudia Muumba wao.

"Tunataka watu wasikae makanisani bali watoke ili nao watoe huduma na kwa kufanya hivyo itasaidia kuonyesha na kunyanyua vipaji na vipawa walivyonavyo katika utumishi wao", alisema Mchungaji Prof. Mbise.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa baada ya kufanya utafiti wamebaini baadhi ya Wilaya katika Mkoa wa Dodoma kama vile Bahi na Kondoa bado watu hawajafikiwa kisawasawa Neno la Mungu hivyo huduma hiyo itawafikia na kuwaondoa katika mnyororo wao.

# Mwarobaini kupanda bei ya nyama huu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KUTOKANA na malalamiko yaliyojitokeza hivi karibuni ya kupanda kwa bei ya nyama nchini, serikali imewashauri wafugaji kuvuna na kuuza mifugo yao ili kukidhi soko lililopo sasa.

Aidha, imesema kuwa malalamiko hayo yanaashiria ukuaji wa sekta hiyo ambapo wafugaji wanatakiwa kuutumia muda huo kufanya biashara ya nyama ili kujikwamua kiuchumi.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alibainisha hayo juzi jijini Dodoma, mbele ya wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Kilimo, Mifugo na Maji wakati wa uwasilishaji wa taarifa ya utendaji kazi wa Bodi ya Nyama nchini.

Ulega alisema kipindi cha nyuma wafugaji walikuwa wakilalamika kutopata masoko ya mifugo yao ila katika kipindi cha sasa uhitaji wa mifugo katika viwanda vya kuchakata nyama umekuwa mkubwa pamoja na hitaji la bidhaa hiyo katika soko la ndani.

"Sekta ambayo ulikuwa hauwezi kuisikia inasemwa, lakini leo inakuwa mjadala hivyo ni wakati mzuri sana kwa wafugaji kuvuna na kuuza mifugo yao." alisema Ulega.

Alisema serikali imetengeneza uhitaji wa nyama baada ya kufungua biashara ya kuuza nyama nje ya nchi, hivyo uhitaji wa mifugo kwenye viwanda vya kuchakata hapa nchini umeongezeka.

Msajili wa Bodi ya Nyama, Dk. Daniel Mushi, aliiambia kamati hiyo kuwa uhaba wa nyama uliojitokeza hivi karibuni na kusababisha bei kupanda ni fursa ya kufuga kibiashara na kunenepesha mifugo.

Alisema kwa sasa sera ya serikali ni kuhamasisha uwapo wa vikundi kwa ajili ya unenepeshaji wa mifugo ili kupatikana kwa mifugo bora kulingana na hitaji la soko la sasa hususani kwenye viwanda vya kuchakata nyama nchini.

Aliongeza kuwa hivi karibuni Tanzania kupitia viwanda vilivyopo nchini itaanza kupeleka nyama katika soko la Saudi Arabia na hitaji la soko hilo ni tani 600,000 kwa mwaka hali ambayo itachangia kwa kiasi kikubwa kukuza sekta ya mifugo nchini.

Akizungumzia kuhusu ugonjwa wa midomo na miguu (FMD) ambao unaathiri mifugo na kusababisha Tanzania kushindwa kupeleka nyama katika baadhi ya nchi Msajili wa Baraza la Veterinari Tanzania (RVCT) Dk. Bedan Masuruli alisema umekuwa ukiathiri biashara ya nje na unasababishwa na uwepo wa wanyama pori.

Alisema ni vigumu kudhibiti ugonjwa huo kwa kuwa Tanzania ina kirusi cha ugonjwa huo ambacho hakipo kwenye chanjo ambazo zinaingizwa nchini kutoka nchi za nje kwa ajili ya kudhibiti ugonjwa na kuna virusi aina saba vya ugonjwa huo.

Akizungumza wakati akihitimisha kikao hicho, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dk. Christine Ishengoma, aliishauri Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuendelea kuisimamia vyema sekta ya mifugo ili kuongeza mapato kwa kuuza mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi.



Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini, Anthony Mavunde (kushoto), akizungumza na Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe (katikati) na Naibu Meya wa Jiji hilo, Emmanuel Chibago, walipokutana katika vikao vya halmashauri, jijini humo juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wanawake wawezeshwa kulima mbaazi

**Na Renatha Msungu**
DODOMA

SHIRIKA la World Vision limetoa mafunzo ya utekelezaji wa kilimo chenye tija kwa wanawake wa Wilaya ya Chemba kuhakikisha wanafanya kilimo bora cha zao la mbaazi.

Akizungumza wilayani humo Joseph Kilimba, mmoja wa waratibu wa mafunzo hayo, alisema lengo ni kuona wanafanya kilimo chenye tija ambacho kitawainua kiuchumi hususani katika zao la mbaazi ambacho kina soko hivi sasa.

Alifafanua kuwa wanahitaji kuona wanakuwa katika kilimo tofauti na ilivyokuwa zamani ili waweze kuingia katika soko la ushindani.

Alisema wanawake wengi wamejikita katika kilimo cha mbaazi ambacho ni kilimo biashara.

"Tuko mstari wa mbele kuhakikisha kilimo kinakua, hivyo tumejipanga kuwainua, "alisema Kilimba.

Hata hivyo alisema mafunzo hayo yewapa manufaa makubwa wanawake kwa sababu hivi sasa wanavuna mbaazi kwa wingi tofauti na ilivyokuwa awali.

Alisema awali walikuwa wakitumia kilimo cha zamani, lakini hivi sasa wameamka na wanafanya kilimo cha biashara.

Aliwataka wanawake wa Wilaya ya Chemba kuangalia fursa zilizopo na wajikite katika kilimo kwa sababu kinalipa.

Aisha Sule aliishukuru World Vision kutokana na msaada inayowapa kwa sababu bila wao wasingefika walipo.

Alifafanua kuwa hivi sasa wana kikundi ambacho kinafanya vizuri kutokana na kilimo cha nyanya, hivyo wanaendelea kukua kila siku.

Alisema wanaendelea kuwashauri wanawake wengine waingie katika kilimo.

Alieleza kuwa hivi sasa kilimo kinalipa na kinawainua kiuchumi jamii zote zinazoishi katika maeneo hayo.



# Jiji lajenga vizimba 270 vya mboga na matunda

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

UBORESHAJI wa Miundombinu ya masoko ya mboga na matunda katika Jiji la Mbeya, umeanza kufanyika, ikiwa kulinda usalama wa chakula na afya za walaji.

Miundombinu hiyo ni pamoja na ujenzi wa vizimba bora kuuzia mboga na matunda, ili kuhakikisha chakula kinachoingizwa na kuliwa jijini Mbeya kinakuwa safi na salama.

Hali kama hii si tu kwa Jiji la Mbeya bali ni kwa masoko mengi yaliyoko katika maeneo mbalimbali nchini, vibanda vilivyotengenezwa kwa mbao vinatajwa kuwa si salama kwa uhakika wa masoko yenyewe.

Masoko ya Soweto, Igawilo na uhindini ni miongoni mwa yanayonufaika na uboreshaji wa miundombinu ya mfano katika Jiji la Mbeya na kwamba kazi ya kuviondoa vizimba hivyo vinaendelea.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akizungumza na Nipashe jana, alisema vizimba 270, vinatarajiwa kujengwa kwenye masoko hayo, ambayo ni ya kimkakati.

"Uboreshaji wa miundombinu hiyo utasadia kuongeza thamani ya mboga na matunda, ili kukidhi vigezo vya walaji wa ndani na nje ya nchi. Licha ya kuongeza thamani ya bidhaa hizo, itasaidia kulinda usalama wa watumiaji kwa sababu itatolewa kwenye mazingira salama," alisema Homera.

Mmoja wa wafanyabiashara wa mboga na matunda, Agnes Isambi, alisema uboreshaji wa miundimbinu ya soko hilo, utapandisha hadi soko na kuonekana la kimataifa hali itakayochangia kupata wateja kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje nchi.

Alisema miundombinu hiyo, itasaidia kukabiliana na majanga ya moto pindi yanapotokea.

Mwenyekiti wa Soko la Soweto, Shadhil Bashiru, aliiomba serikali kwa kushirikiana na Shirika la Ricolto, kujenga vizimba vya bidhaa zingine sokoni hapo na si tu mboga na matunda kama ilivyofanyika kwa sasa.

Alisema miundombinu ya vizimba kwa wafanya biashara sokoni hapo ikiboreshwa, itachangia kuongeza pato kwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya na wajasiriamali kujikwamua kiuchumi.

Mratibu wa Mradi wa Agriconnect kupitia shirika la Ricolto, Shukuru Tweve, alisema ni mradi wa mboga na matunda unaotekelezwa katika mikoa mitano ya Nyanda za Juu Kusini, ambayo mbali na Mbeya ni Songwe, Iringa, Rukwa na Katavi.

Alisema vizimba vya mbao ambavyo vilikuwa vikitumika awali vilikuwa kikwazo katika kupata mikopo kwenye taasisi za kifedha na kwamba vizimba hivyo vipya, ambavyo vimejengwa kisasa vitasaidia kupata mikopo.

Mradi huo wa ujenzi wa vizimba vya kisasa vya mboga na matunda, unasimamiwa na Ricolto kwa kushirikiana na Chama Cha Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) Mkoa wa Mbeya kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU).



Ujenzi wa vizimba vya wajasiriamali zaidi ya 200, ukiendelea katika soko la Soweto jana, ikiwa ni utekelezaji wa mradi wa mboga na matunda unaosimamiwa na shirika la Rikolto kwa kushirikiana na Chama cha Wafanyabiashara wa Viwanda na Kilimo (TCCIA) jijini Mbeya. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Dk. Tulia amwaga mikopo bodaboda

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

TAASISI ya Tulia Trust imetoa mkopo wa bodaboda 21 zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 50 kwa vikundi mbalimbali vya waendesha bodaboda katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Kwa mujibu wa Meneja wa Tulia Trust, Jacqueline Boaz, mikopo hiyo ni mwendelezo wa utaratibu wa taasisi hiyo kuendelea kuwasaidia wananchi wa Jiji la Mbeya kujikwamua kiuchumi hususani vijana.

Boaz alisema baadhi ya vijana wa bodaboda walianza na mkopo wa Sh. 200,000 baada ya marejesho kuwa mazuri, walifikia Sh. 800,000 na kuwawezesha kupata fursa ya kukopa vyombo vya usafiri zikiwamo bodaboda na bajaji.

"Kupitia Tulia Trust tumewasaidia wananchi wa maeneo mbalimbali ya jiji la Mbeya kujikwamua na umasikini kwa kupata mitaji na kufanya shughuli za kuwaingizia kipato ndiyo maana siku hizi vitendo vya uhalifu ikiwamo wizi vimepungua. Hii ni kwa sababu watu wako 'bize' kujitafutia riziki," alisema.

Meneja huyo alisema anaamini hata bodaboda walizokopeshwa zitaendelea kuimarisha uchumi wa vijana na kwamba wataendelea kutoa mikopo ya fedha na vyombo vya usafiri ili vijana watimize ndoto zao.

Akipokea mkopo huo kwa niaba ya wanachama, Mwenyekiti wa Bodaboda Jiji la Mbeya, Aliko Fwanda, aliishukuru Tulia Trust kwa kutoa mikopo yenye riba nafuu ambayo imesaidia kumiliki pikipiki badala ya kuendelea kuendesha pikipiki za watu.

Mmoja wa wanufaika na mkopo huo, Paul Christopher, alisema wamekubaliana kurejesha mkopo huo kwa wakati ili kutoa fursa kwa wengine kupata huduma hiyo.

# Wataka tathmini athari za mazingira bomba la mafuta Uganda hadi Tanga

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

WADAU wa Mazingira nchini wameiomba Serikali kuendelea kufanya tathmini ya kutosha juu ya athari za mabadiliko ya tabianchi na madhara yanayoweza kutokea baada ya kukamilika na kuanza kutumika kwa mradi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi hadi Chongoleani, Tanga.

Sambamba na hilo, wadau hao wameiomba serikali kuwalipa fidia wakazi wote waliopisha mradi huo ili kupata makazi na maeneo ya kuendeleza shughuli zao za kilimo na ufugaji.

Mratibu wa Taasisi ya Green Faith International Tanzania, Baraka Lenga, amesema jana kuwa utafiti unaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 90 ya mabadiliko ya tabianchi yanasababishwa na shughuli za kibinadamu ambazo zinachangia ongezeko la gesi joto duniani.

Alisema utafiti huo uliofanywa na jopo la wanasayansi wa kimataifa wanaoshughulika na suala la mabadiliko ya tabianchi (Intergovernmental Panel on Climate Change -IPCC) unaonyesha kuwa miongoni mwa mambo yanayosababisha ongezeko la gesi joto ni nishati.

"Tanzania na Uganda kuna mradi wa bomba la mafuta ghafi unaoendelea. Kwa kuwa nasi ni wadau muhimu wa mazingira, tulitembelea eneo la mradi huo jijini Tanga kuangalia ni kwa namna gani utakuwa na manufaa kwa wananchi ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Pia tuliangalia ni kwa namna gani wananchi wanaweza kuathirika na kutoa ushauri wa namna bora ya kuepukana na athari za kiafya na kimazingira," alisema Lenga.

"Miongoni mwa mambo tuliyoyaona kwa wananchi waliopisha mradi huo, wengi wao wamechukuliwa ardhi ambayo walikuwa wakiitumia kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji na kwamba fidia waliyoipata hawajaridhishwa nayo," aliongeza.

Pia alisema baadhi ya wananchi walihojiwa wanasema walilipwa fidia za kupisha mradi huo na wengine bado wanadai stahiki hiyo haikidhi kupata eneo lingine kwa ajili ya makazi na kuendesha shughuli za uzalishaji mali.

Lenga anasema licha ya mradi huo kuendelea kufungua fursa za ajira kwa wananchi na kuinua uchumi kwa wafanyabiashara, ni muhimu kukazingatiwa suala la mabadiliko ya tabianchi kwa sababu kuna miti iliyofyekwa ambayo kimsingi inasaidia kufyonza gesi joto ambayo huitwa hewa ukaa ambayo ikiongeza katika anga hewa, huathiri mfumo wa hali ya hewa na kusababisha ongezeko la joto duniani.

Rais Samia Suluhu Hassan na Yoweri Museveni wa Uganda, Aprili, mwaka huu, walitia saini rasmi mkataba wa utekelezaji wa mradi wa kujenga bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima, magharibi mwa Uganda hadi bandari ya Tanga.

Mradi huo una thamani ya Dola za Marekani bilioni 3.5 na umbali wa kilomita 1,440 na utapita kwenye mikoa minane ya Tanzania Bara. Mradi huo unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 36 na kuzalisha ajira takriban 15,000.



# Mganga wa jadi jela miaka 30 kwa kubaka

**Na Mwandishi Wetu** PEMBA,

MAHAKAMA ya Mkoa Chakechake Pemba imemhukumu Mshitakiwa Issa Abdalla Haji (41), ambae ni mganga wa kienyeji mkazi wa Shehia ya Wawi miaka 30 jela pamoja na kulipa fidia ya Sh. 1,000,000 baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kubaka.

Hukumu hiyo imetolewa juzi na Hakimu wa Mahakama hiyo, Luciano Makoye Nyengo, baada ya mtuhumiwa kukiri kutenda kosa.

Kabla ya hukumu, Mwendesha Mashtaka Ali Amour Makame kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka alidai kwamba mshtakiwa alimbaka mwanamke (39).

Imedaiwa Oktoba 11, mwaka huu mshitakiwa alimtaka mwanamke huyo ambaye ni mteja wake aliefuata huduma afanye naye mapenzi ikiwa ni miongoni mwa masharti ya dawa itakayoweza kutatua tatizo lake ambalo alimueleza mganga huyo.

Ilidaiwa mteja huyo alifika kwa mganga huyo ili kutatuliwa tatizo lake ambalo mume wake aliwekwa rumande akishikiliwa kwa tuhuma ya kesi ya jinai, hivyo aliamini kuwa mganga huyo angempatia dawa za kumtoa mume wake rumande.

Ilidaiwa mshtakiwa alimbaka mwanamke huyo jambo ambalo ni kosa kisheria kwa mujibu wa sheria za Zanzibar ya mwaka, sheria namba 6 ya mwaka 2018.

Mshitakiwa alipotakiwa kujibu shitaka hilo, alikiri kutenda kosa hilo, ndipo Hakimu Makoye Nyengo alipomuamuru kutumikia kifungo cha miaka 30 jela na kumlipa mlalamikaji fidia ya Sh. milioni moja ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia

**Imedaiwa Oktoba 11, mwaka huu mshitakiwa alimtaka mwanamke huyo ambaye ni mteja wake aliefuata huduma afanye naye mapenzi ikiwa ni miongoni mwa masharti ya dawa itakayoweza kutatua tatizo lake ambalo alimueleza mganga huyo.**

# Sheria dawa za kulevya sasa kurekebishwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar , Othman Masoud Othman, amesema Serikali ya Zanzibar inaifanyia marekebisho sheria ya Dawa za Kulevya Zanzibar.

Makamu huyo aliyasema hayo jana huko Kidimni Wilaya ya Kati Unguja alipofanya ziara ya kukagua Kituo cha Kurekebisha Tabia kwa vijana walioathirika na dawa za kulevya.

Othman alisema hatua hizo zinatokana na ukweli kwamba dawa za kulevya Zanzibar bado ni tatizo kubwa linalohitaji mpango madhubuti wa kitaifa utakaosaidia kuweka mfumo na utaratibu bora wa mapambano hayo.

Alisema kwamba sheria hiyo ambayo inatarajiwa kupitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar katika Mkutano ujao inatarajiwa kuweka miundombinu imara na itakuwa ni nyenzo madhubuti ya kufanyia kazi dhidi ya tatizo la dawa za kulevya nchini.

Alisema kwamba mageuzi hayo ya sheria pia yatasaidia serikali kulipatia ufumbuzi suala la muhali ambayo imekuwa ikichangia sana kuharibu juhudi na uwezo wa mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini.

Aidha alisema katika hatua za kukabiliana na changamoto mbalimbali za kupambana na dawa za kulevya Zanziba kutaandaliwa mpango mkuu wa kitaifa wa kupambana na dawa za kulevya utakaoainisha mgawanyo bora wa majukumu kwa taasisi na wadau mbalimbali wanaoshiriki katika mapambano hayo.

Alisema kwamba suala hilo litashirikisha kila mdau na taasisi zote nchini ikiwa ni sehemu ya mkakati sahihi kwa kila mhusika kuandaa mpango kazi wake wa utekelezaji utakaolenga kumaliza tatizo la dawa za kulevya Zanzibar.

Mkurugenzi wa Tume ya Kitaifa ya Kudhibiti na Kuratibu Dawa za Kulevya Zanzibar, Kanal Burhan Zubeir Nassor, alisema kwamba tume yake inakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazokwamisha juhudi za mapambano hayo.

Alizitaja baadhi ya changamoto hizo kuwa ni pamoja na kesi kukaa muda mrefu bila kuchukuliwa hatua na kukamilika, kutopatikana mashahidi mahakamani na kesi kufutwa licha ya juhudi kubwa zilizochukuliwa kuwakamata washitakiwa.

Hata hivyo, alisema kwamba mageuzi ya sheria kuhusu suala la dawa za kulevya yanayopendekezwa yatasaidia kukabili suala la muhali na mambo mengine ambayo yamekuwa yakichangia sana kuharibu juhudi za mapambano dhidi ya madawa ya kulevya Zanzibar.




Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said (katikati), akitia saini hati ya makubaliano ya msaada wa kuwarejesha shule wanafunzi watoro, nchini Qatar jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Qatar Fund For Development (QFFD), Khalifa Al Kuwari na Balozi wa Tanzania nchini Qatar, Mahadhi Juma Maalim. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watendaji waagizwa kurejesha watoto shule

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya Kati Unguja, Marina Joel Thomas, amewataka watendaji wa Mkoa wa Kusini Unguja kuhakikisha wanasimamia ipasavyo kuwarejesha wanafunzi walioacha masomo katika maeneo mbalimbali ili kupata haki yao ya msingi.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja katika Ofisi ya Mkoa iliyopo Tunguu katika kikao kilichowashirikisha watendaji na wadau wa elimu chenye lengo la kutoa uelewa juu ya suala zima la watoto ambao wameacha shule chini ya umri wa miaka saba hadi 14.

Alisema imebainika kwamba katika Mkoa wa Kusini Unguja kuna idadi kubwa ya watoto waliotoroka shule na zaidi ya watoto wapatao 1,500 wameacha masomo kwa visingizio tofauti ikiwamo ya kuachana kwa wazee, umasikini na utoro.

Alisema mradi huu wa kuwarejesha wanafunzi shule ulioanzishwa na Wizara ya Elimu utasaidia kuendelea na masomo yao ili lengo la kuazishwa mradi huo liweze kufikiwa .

Aidha aliwataka wazazi kuwapa ushirikiano walimu na kuwa karibu kwa kufuatilia mienendo za watoto wao ili kuwanusuru na vitendo vya udhalilishaji ambao umekuwa kero kwa taifa sambamba na kuwa mstari wa mbele katika maendeleo ya elimu ya watoto wao ili kubaini mapema matatizo mbalimbali yanayoweza kujitokeza.

Naye Mkurugenzi Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima, Mashavu Ahmada Fakihi na Mratibu wa mradi wa kurejesha watotos, Mzee Shirazi Hassan, walisema tangu kuanza kazi ya kuhamasisha mradi huo jamii imepata mwamko na watoto wameanza kurudi mashuleni, hivyo watendaji waliopatiwa mafunzo wanapaswa kuitumia elimu ipasavyo na kuifikisha kwa jamii husika.

Washiriki wa kikao hicho walisema kukosekana kwa malezi ya pamoja kunapelekea kwa kiasi kikubwa kuporomoka kwa maadili ya watoto wao hivyo hali ya umasikini isiwe ni kigezo cha kuwakosesha haki ya kupata elimu watoto.

## HABARI KIMATAIFA

## Mtalii ashuhudia tembo akiua mamba mtoni

**Lisaka,** ZAMBIA

MTALII akiwa kwenye safari mbugani, alipiga picha ya video wakati mamba akikanyagwa hadi kufa na tembo, baada ya kumnyemelea mtoto wake kwenye mto nchini Zambia.

Kwenye video hiyo, tembo alimshambulia mamba huyo kwa nguvu kutumia kichwa chake, kabla ya kumkanyaga katika mto huku kundi la watalii likiangalia.

Tukio hilo nadra, lilinaswa na Hans Henrik Haahr na limewekwa mtandaoni na Latest Sightings, idhaa ya YouTube inayoziweka video za wanyamapori zilizorekodiwa kote Afrika.

"Tembo kwa kawaida ni wanyama wenye amani na wanaojali sana, hata hivyo, tembo wa kike wanaweza kuwa wakali wakati wa kulinda ndama mchanga," Latest Sightings alisema.

Hans, alisema alikuwa hana maneno ya kuelezea tukio hilo na kwamba lilikuwa la kushangaza.

Kukanyagwa huko kulisababisha kifo cha mamba.

**BBC**

# WHO: Corona bado ipo hadi 2022

**New York,** MAREKANI

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limesema janga la Covid-19 litaendelea kwa mwaka zaidi ya inavyotakiwa, kwa sababu nchi maskini hazipati chanjo zinazohitajika,

Dk. Bruce Aylward, kiongozi mwandamizi wa WHO, amesema inamaanisha kwamba janga la Covid-19 linaweza kufika hadi mwaka 2022.

Chini ya asilimia tano ya idadi ya watu wa Afrika wamepewa chanjo, ikilinganishwa na asilimia 40 katika mabara mengine.

Uingereza imetoa chanjo zaidi ya milioni 10 kwa nchi zinazohitaji na imeahidi kutoa jumla ya milioni 100.

Dk. Aylward alitoa wito kwa nchi tajiri kutoa nafasi zao kwenye foleni ya chanjo ili kampuni za dawa kutanguliza nchi zenye kipato cha chini.

Janga la Covid-19 lilikuwa linazuilika, jopo huru la ukaguzi lilisema, lililoundwa na WHO.

Limesema maandalizi ya pamoja ya WHO na serikali duniani kujibu janga hilo yalikuwa mseto wenye sumu.

Jopo lilisema WHO ilipaswa kutangaza hali ya dharura duniani mapema, kuliko ilivyofanya, na kuongeza kuwa bila mabadiliko dunia ilikuwa hatarini kwa mlipuko mwingine mkubwa wa magonjwa.

Zaidi ya watu milioni 3.3 kote duniani sasa wamekufa kutokana na virusi vya corona.

Marekani na Ulaya zilipoanza kupunguza vizuizi na kuanza kurejea maisha ya kabla ya janga, virusi hivyo bado vinaangamiza sehemu za Asia.

Ripoti hiyo ya Covid-19, ilisema liwe ndilo janga la mwisho, na kuwapo mbinu jinsi ya kukabiliana nalo.

Lengo lake lilikuwa kupata majibu ya jinsi virusi hivyo vilivyoua zaidi ya watu milioni 3.3 na kuambukiza zaidi ya milioni 159.

"Hali tunayojikuta leo ingeweza kuzuiwa," mwenyekiti mwenza Ellen Johnson Sirleaf, rais wa zamani wa Liberia, aliwaambia waandishi wa habari.

"Ni kwa sababu ya kutofaulu, mapungufu na ucheleweshaji wa utayari na majibu."

Jopo hilo lilisema kwamba Kamati ya Dharura ya WHO ilipaswa kutangaza kuzuka huko China kuwa dharura ya kimataifa wiki moja mapema kuliko ilivyofanya.

Ilipaswa kufanya hivyo katika mkutano wake wa kwanza Januari 22, mwaka jana, ripoti ilisema, badala ya kungojea hadi Januari 30.

Mwezi uliofuata tamko la WHO kuhusu hatari ya corona ulipotea wakati nchi zilishindwa kuchukua hatua zinazofaa ili kukomesha kuenea kwa virusi.

Wakati huo WHO ilibanwa na kanuni zake kwamba vizuizi vya kusafiri vinapaswa kuwa suluhisho la mwisho, jopo lilisema kuwa Ulaya na Marekani, zilipoteza mwezi mzima wa Februari na zilichukua hatua tu wakati hospitali zao zilipoanza kujaa.

Wakati nchi zilipopaswa kuwa zinaandaa mifumo yao ya afya kuwashughulikia wagonjwa wa Covid-19, sehemu kubwa ya dunia ilikuwa iking'ang'ania vifaa vya kujikinga na dawa, ilisema ripoti hiyo.

Dk. Aylward alitoa wito kwa nchi tajiri kutoa nafasi zao kwenye foleni ya chanjo, ili kampuni za dawa zianze na nchi zenye kipato cha chini. **BBC**

## Rusesabagina akata rufani hukumu yake

**Kigali,** RWANDA

WAENDESHA mashtaka wamewasilisha rufani dhidi ya uamuzi wa korti juu ya Paul Rusesabagina, mtu aliyeonyeshwa kama shujaa katika sinema ya Hollywood kuhusu mauaji ya kimbari ya Rwanda.

Rusesabagina (67), alihukumiwa kifungo cha miaka 25 jela mwezi uliopita baada ya kupatikana na hatia ya kuunga mkono kundi la waasi lililohusika na mashambulio mabaya mwaka 2018 na 2019.

Waendesha mashtaka wa Rwanda, walikuwa wametaka apewe kifungo cha maisha na walikuwa wameonyesha kutofurahishwa na uamuzi wa kutoa adhabu nyepesi kuliko walivyotaka.

Rusesabagina alikuwa amejiondoa kwenye kesi hiyo, ambayo vikundi vya haki, wafuasi na familia yake waliitaja kama kandamizi.

Korti ya rufani, inapaswa kuamua baadaye tarehe ambayo itaanza kusikiliza rufani hiyo.

**BBC**


## Ushauri wa Wadau wa Mitaa kwa shughuli za mradi wa kaboni ya Dhahabu 'RUDI WATER Project'

4ife

**Ndugu Mdau,**

4LIFE Solutions itatekeleza shughuli za mradi wa kaboni VPA2: 'RUDI WATER Project' chini ya Mpango wa Shughuli za Kiwango cha Dhahabu (PoA) Programu endelevu ya Usafi wa Maji. Mradi utasambaza teknolojia salama ya utakaso wa maji, inayoitwa SaWa, kulingana na Teknolojia inayotumia miale ya jua ili Kuzuia Maambukizi ya magonjwaa/maambukizi yanayotokana na unywaji Maji yasiyo masafi kwa kaya zinazoishi katika mikoa ya Shinyanga na Ruvuma (Madama, Namtumbo, Songea, Kahama / Msalala, Shinyanga DC, MbogweWilaya), Tanzania. PoA inasimamiwa na 4Life Solutions (zamani inayojulikana kama SolarSack), iliyo na ofisi kuu Kidenmaki inaanza. Katika muktadha huu Ushauri wa Umma wa Wadau wa Mitaa utafanyika kwa wadau wote wa ndani ya nchi, walioathirika na wanaovutiwa, pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali, vikundi vya wanawake, taasisi za utafiti na mashirika / watu wanaofanya kazi juu ya mada zinazohusiana na shughuli za mradi, watunga sera juu ya kitaifa na ngazi ya wilaya na pia kwa watu wa eneo, jamii na wawakilishi ambao wameathiriwa moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja na mradi huo.

4LIFE Solutions (Waratibu na wasimamizi Taasisi ya PoA) inaalika watu wote wanaopenda kuhudhuria
**Ushauri wa Wadau wa Mtaa mnamo Oktoba 29th, 2021, 8:30 asubuhi hadi 13:00 jioni katika**
**Ruhuwiko Hunt Club**
**Mji wa Ruhuwiko-Songea**
**Mbinga road**
**Tel N ° ya ukumbi+255620655773 AU +255252951008**

Wadau ambao hawawezi kuhudhuria mkutano huo, wana uwezekano wa kushiriki mkondoni kupitia Zoom. Maelezo ya kuingia ni yafuatayo:

Umealikwa kwenye mkutano wa Zoom.
**Wakati: Oktoba 29, 2021 08:30 AM E.A.T (MUDA WA AFRIKA MASHARIKI)**

Jisajili mapema kwa mkutano huu ukitumia kiunga hiki:
**https://us02web.zoom.us/meeting/register/tZAsfuivqT8pG9FuSHs5itwOHbQDg7-5ZN1U**

Baada ya kujiandikisha, utapokea barua pepe ya uthibitisho iliyo na habari juu ya kujiunga na mkutano huo.

### AJENDA

- **Mapokezi - Kutia saini orodha ya washiriki (8:30 asubuhi)**
- **Utangulizi na uwasilishaji wa Mradi (9:00 asubuhi)**
- **Maswali na maoni juu ya mradi huo (9:30 asubuhi)**
- **Kanuni za Kulinda Tathmini ya mradi (10:30 asubuhi)**
- **Tathmini endelevu ya mradi (11:15 am)**
- **Majadiliano juu ya utaratibu wa malalamiko na ufuatiliaji wa athari za maendeleo endelevu (12:15 pm)**
- **Fomu za tathmini na kufungwa kwa mkutano (12:30 pm)**
- **Maonyesho (12:45 pm)**
- **Chakula cha mchana (13:00 pm)**

11652601

**www.4lifesolutions.com**

Ikiwa kuna maswali yoyote au ikiwa unataka maelezo zaidi na habari za mradi kabla ya mashauriano, tafadhali andika barua pepe kwaJulius Macharia, Meneja wa Kaboni kutoka 4LIFE Solutions (jkm@4lifesolutions.com) au piga simu kwa Happiness Urasa, Msimamizi wa Miradi nchini Tanzania kutoka 4Life Solutions (+255 767 007 505) Tafadhali tumia maelezo haya ya mawasiliano pia kwa kutoa maoni yako ikiwa huwezi kushiriki katika mkutano wa wadau.

HABARI MICHEZO

# SHIME AFUNGUKA TWIGA STARS WAKIIFUATA NAMIBIA SAUZI

**Na Saada Akida**

BAADA ya kikosi chake kukubali kipigo cha mabao 2-1 nyumbani dhidi ya Namibia, Kocha Mkuu wa Twiga Stars, Bakari Shime, amesema kutocheza kwa kiwango bora ambacho kimezoeleka ni sababu kubwa ya wao kupoteza mchezo huo wa kwanza kwao kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) kwa wanawake, zitakazofanyika mwakani nchini Morocco.

Twiga Stars ambayo iliondoka jana alfajiri kuelekea Afrika Kusini tayari kwa mchezo huo wa marudiano, ilikubali kichapo hicho juzi katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mechi hiyo ya marudiano itapigwa Afrika Kusini kesho, Jumamosi katika Uwanja wa Dobsonville, Soweto, hivyo licha ya Namibia kuwa wenyeji, timu zote zitakuwa kama zipo ugenini jambo ambalo ni faida kwa Twiga Stars.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mchezo huo, huku akiwapongeza wapinzani wao kwa ushindi huo, Shime alisema anafurahi mechi hiyo imeisha salama na hakuna majeruhi katika kikosi chake.

Alisema sababu kubwa ya wao kutopata matokeo katika uwanja wa nyumbani ni ubora wa mbinu za wapinzania wao pamoja na timu yake kutokuwa katika ubora ambao wamekuwa wakiuonyesha.

"Hatukuwa na ubora wetu, lakini hatukucheza vibaya, tulitengeneza nafasi nyingi hatukuweza kuzitumia, lakini wapinzani wetu walitengeneza nafasi mbili na kufanikiwa kupata idadi ya mabao hayo," alisema Shime.

Alisema hata 'kombinesheni' ya washambuliaji wake kati ya Opa Clement na Aisha Masaka haikuwa nzuri pamoja na timu kwa ujumla kwa sababu ya yaliyotokea Afrika Kusini baada ya kuibuka na ubingwa wa COSAFA.

"Tuliporejea kutoka Afrika Kusini, nilisema licha ya kurejea na kombe, lakini sina furaha kwa sababu ya madhara, majeruhi, 'fatigue' (uchovu) pamoja na furaha waliyokuwa nayo (wachezaji) kusababisha kisaikolojia kuchelewa kurejea kwenye kiwango chetu bora.

"Tunapokea matokeo haya na kurudi uwanjani kwa ajili ya kuendelea kupambana kwa hali yoyote kuhakikisha tunarudia kwenye ule ubora ambao tulikuwa tukionyesha nyuma kwa ajili ya mchezo wetu wa marudiano," alisema Shime.

Alisema sasa wanaenda kujipanga na kusahihisha makosa yao na kupambana kuwarejesha wachezaji kisaikolojia ili kupata matokeo mazuri katika mchezo huo wa marudiano utakaopigwa nchini Afrika Kusini kesho.

"Tuna imani ya kufanya vizuri katika mchezo wetu wa marudiano na kupata matokeo mazuri na kuendelea kusonga mbele katika michuano hii," alisema Shime.



Mshambuliaji wa Twiga Stars, Opa Clement (Kulia), akipata upinzani mkali dhidi ya mabeki wa Namibia kwenye mechi ya kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) kwa wanawake zitakazofanyika mwakani nchini Morocco. Katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, Twiga Stars ilikubali kipigo cha mabao 2-1. **MPIGAPICHA WETU.**

# KMKM, Mafunzo kukinukisha Ngao ya Jamii J'mosi

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MSIMU mpya wa Ligi Kuu Zanzibar unatarajiwa kufunguliwa Jumamosi kwa mabingwa watetezi wa ligi hiyo, KMKM kushuka dimbani dhidi ya bingwa wa Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (FA Cup), Maafande wa Mafunzo katika mchezo wa Ngao ya Jamii utakaopigwa Uwanja wa Amaan visiwani hapa majira ya saa 11:00 jioni.

Mechi hiyo ambayo ni maalum kwa ajili ya kukaribisha msimu mpya wa 2021/22, imedhaminiwa na Shirika la Bima Zanzibar, na baada ya mchezo huo, rasmi sasa Ligi Kuu visiwani hapa itaanza kutimua vumbi Jumatatu ijayo, Oktoba 25.

Akizungumza na gazeti hili jana kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, alisema matarajio yao ni kuhahikisha wanapata ushindi wa mwanzo wa msimu na kuanza na taji.

Alisema tayari wamefanya maandalizi na wamejiandaa kupata matokeo mazuri katika mchezo huo ambao utakuwa na upinzani mkali kutokana na historia ya timu hizo zinapokukutana katika Ligi ya Zanzibar na michezo mingine.

Alisema katika mchezo huo atawatumia nyota wake wapya waliosajiliwa msimu huu pamoja na wachezaji wake wazamani.

"Kuelekea mchezo huu muhimu, tumecheza michezo miwili ya kirafiki na timu za hapa hapa nyumbani Zanzibar, mechi hizi lengo ni kuangalia wapi pana mapungufu tupafanyie kazi, jambo ambalo tayari tumeshafanyia kazi,"alisema.

Msimu uliopita Ligi Kuu Zanzibar ilijumuisha timu 12, lakini msimu huu zitakuwa 16 huku mwishoni mwa kinyang'anyiro hicho, nne zikishuka daraja na idadi kama hiyo zikipanda ambapo mbili zitapanda kutoka Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja na mbili Kanda ya Pemba. Msimu huu zilishuka timu mbili na kupanga sita.

Ratiba ya mechi za ligi hiyo, inayoanza Jumatatu, ilitarajiwa kutolewa jana na Bodi ya Ligi Zanzibar.

## Biashara yapania ushindi kwa Walibya

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa wawakilishi wa Tanzania katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Biashara United, Patrick Odhiambo, amesema ana matarajio makubwa ya kupata matokeo chanya ugenini katika mchezo wao wa marudiano dhidi ya Al Ahli Tripoli ya Libya utakaopigwa kesho.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana kabla ya kuondoka kuelekea Libya, Odhiambo alisema baada ya kusahihisha makosa yao, ikiwamo viungo na mabeki, ana matarajio makubwa ya kufanya vizuri katika mchezo huo wa marudiano.

Alisema anapambana kuhakikisha anawaandaa vizuri wachezaji wake kisaikolojia, kwa sababu ya changamoto watakazokutana nazo katika msafara wao ili usiwaondoe morali waliyokuwa nayo kuelekea mechi hiyo.

"Mechi itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu wenzetu wako nyumbani wanahitaji kupata matokeo mazuri, kwa upande wetu pia tunahitaji kufanya vizuri ili kusonga mbele katika michuano hii.

"Tunafaida ya ushindi wa mabao mawili tuliopata nyumbani, lakini hayatufanyi kuridhika. Tunaenda kucheza mchezo wa marudiano kwa nidhamu na tahadhari kubwa ili kufikia malengo yetu," alisema Odhiambo.

Biashara United inahitaji ushindi ama sare yoyote au kutokubali kupoteza zaidi ya bao 1-0, ili kusonga mbele kwenye michuano hiyo kutokana na faida ya ushindi wa mabao 2-0 walioupata nyumbani.

## Taifa Queens kambini kujiandaa kimataifa

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya mchezo wa Netiboli, Taifa Queens, inatarajia kuingia kambini kesho, Jumamosi kwa ajili ya kujiandaa kwenda kushiriki mashindano ya kimataifa yatakayoanza kutimua vumbi kuanzia Novemba 8-16, mwaka huu nchini Namibia, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Chama cha Mchezo nchini (Chaneta), Devota Marwa, alisema maandalizi kwa ajili ya mashindano hayo yanaendelea vizuri huku akitoa shukurani kwa wadau wote ambao wamewasaidia mpaka kupata kambi hiyo.

"Jumamosi (kesho), timu yetu inatarajia kuingia kambini kwa ajili ya kujiweka sawa kuelekea katika mashindano hayo ambapo mazoezi yetu tutakuwa tunayafanya kwenye viwanja vya JKT Mgulani na ndipo mahali kambi ilipo," alisema Marwa.

Alisema timu hiyo itaondoka nchini kuelekea Namibia Novemba 7, mwaka huu, na kuziomba taasisi mbalimbali ziendelee kuwaunga mkono ili safari yao ifanikiwe.

## ZISIKUPITE

### DEMBELE TAYARI NEWCASTLE

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Ousmane Dembele, yuko tayari kuhamia Newcastle United wakati mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu. Nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 24, alijiunga na klabu hiyo ya Catalunya kwa ada ya pauni milioni 117 mwaka 2017. **(Goal)**

### MARTINEZ, GERRARD WAMULIKWA

WAMILIKI wapya wa Newcastle bado hawajafikia uamuzi wa mwisho kuhusu kocha wa kumuajiri, huku kocha wa timu ya Taifa ya Ubelgiji, Roberto Martinez, Frank Lampard, Lucien Favre, Steven Gerrard na Eddie Howe bado wakiendelea kufuatiliwa. **(Guardian)**

### HAALAND ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA wanamtaka mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21 kutoka Borussia Dortmund, amesema kocha wa timu hiyo, Thomas Tuchel. **(Bild via The Sun)**

### VLAHOVIC AWANIWA CITY

KLABU ya Manchester City wanamsaka mshambuliaji wa Fiorentina, Mserbia Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 21. **(Tuttosport via Manchester Evening News)**

### OLMO AGOMBEWA MANCHESTER

KLABU ZA Manchester City na wapinzani wao wa jiji moja, Manchester United, wanafikiria kuchuana na Barcelona katika mbio za kusaka saini ya mshambuliaji wa RB Leipzig na Hispania, Dani Olmo. **(Christian Falk on Twitter)**

### TIELEMANS AKATAA OFA

KIUNGO wa Leicester City, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 24, amekataa ofa ya kuongeza mkataba, na kuzifanya klabu za Manchester United, Chelsea, Liverpool, Real Madrid, Atletico Madrid na Bayern Munich kukaa mguu sawa. **(90 mins)**

### ONUACHI ATAJWA SPURS

Tottenham Hotspur imejiunga katika orodha ndefu ya klabu ikiwamo West Ham, kumfuatilia mshambuliaji wa Genk, Paul Onuachu. Klabu yake hiyo ya Ubelgiji inataka ada ya pauni milioni 20 ili kumuachia raia huyo wa Nigeria mwenye urefu wa zaidi ya futi sita. **(Daily Mail)**

### BAYO ATAKIWA BRIGHTON

KLABU ya Brighton wanamfuatilia mshambuliaji wa Clermont raia wa Guinea, Mohamed Bayo mwenye umri wa miaka 23, ambaye klabu yake hiyo ya Ufaransa inataka ada ya pauni milioni 10, Bayo amekuwa akifananishwa na straika wa Chelsea, Romelu Lukaku. **(Argus)**

### FERNANDES NA MKWALA UNITED

KIUNGO Bruno Fernandes mwenye umri wa miaka 27, alitishia kuondoka baada ya kusikia klabu yake ya Manchester United ilikua moja ya klabu 12 zilizosaini mpango wa kuanzishwa kwa ligi mpya ya Ulaya. **(The Athletic)**

### DYBALA KUJIFUNGA JUVE

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Paulo Dybala mwenye umri wa miaka 27, anakaribia kusaini mkataba mpya na vigogo wa Italia, Juventus, amesema makamu wa rais wa klabu hiyo, Pavel Nedved. **(Football Italia)**

### FONSECA HUYOOO NEWCASTLE

NEWCASTLE imemfanyia usaili kocha wa zamani wa Roma, Paulo Fonseca, kupitia njia ya mtandao wa Zoom, mreno huyo mwenye umri wa miaka 48, anaonekana kuongoza katika makocha wanaowaniwa kumrithi, Steve Bruce. **(Daily Mail)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO AKUNWA NA MORALI KIKOSINI UNITED

Sisi ni Man United na kamwe hatukukata tamaa, hapa ndio Old Trafford, ndoto yetu ipo hai, tuko pamoja...

**MANCHESTER, England**

CRISTIANO Ronaldo amesifia morali wa Manchester United wa kupambana hadi mwisho baada ya kufunga bao la ushindi wakati wakitoka nyuma na kushinda mabao 3-2 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Atalanta, Jumatano.

United walikuwa nyuma kwa 2-0 kipindi cha kwanza kwa mabao ya Mario Pasalic na Merih Demiral kwenye mchezo huo wa Kundi F pale katika dimba la Old Trafford kabla ya Ronaldo kufunga la ushindi dakika ya 81.

Ilikuwa ni mara ya tatu kwa 'Mashetani Wekundu' hao kushinda mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakitoka nyuma kwa mabao mawili.

"Ndio! Ndoto yetu ipo hai! Tuko pamoja!," aliandika Ronaldo kupitia kwenye mtandao wake wa kijamii.

"Sisi ni Man United na kamwe hatukukata tamaa! Hapa ndio Old Trafford!"

Bao la Ronaldo lilikuja baada ya Marcus Rashford na Harry Maguire kuisawazishia Man United.

Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, amefunga mara sita kwenye mechi sita za mashindano yote tangu aliporudi United kutoka Juventus Agosti mwaka huu.

Mabao ya Pasalic na Demiral ya kipindi cha kwanza, yalimaanisha kwamba, United walikuwa nyuma kwa 2-0 ndani ya dakika 29, ambapo iliwafanya Mashetani Wekundu hao kufungwa kwa haraka zaidi kwenye Uwanja wa Old Trafford kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza tangu Oktoba 2012, wakati walipokuwa nyuma na kushinda 3-2 dhidi ya Braga.

MECHI KALI
HOME AWAY
ARSENAL
1.98 | 3.54 | 3.74
ASTON VILLA

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 595

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# UMTITI NA MACHOZI MBELE YA LAPORTA



**BARCELONA, Hispania**

MLINZI wa Barcelona, Samuel Umtiti alimwaga machozi mbele ya Rais wa klabu hiyo, Joan Laporta, wakati walipokutana kujadili kuhusu hatima yake ndani ya timu hiyo.

Umtiti amefichua siri hiyo yeye mwenyewe akielezea namna anavyopitia wakati mgumu klabuni hapo chini ya kocha wa sasa, Ronald Koeman aliyechukua mikoba hiyo msimu uliopita.

Beki huyo hajacheza mchezo wowote hadi sasa ndani ya msimu huu akiwa chini ya Koeman, majeraha pia yalichangia mchezaji huyo kukosa namba katika kikosi cha kwanza.

"Nililia mbele ya rais kwa sababu nafahamu yeye anajua mimi ni nani," alisema Umtiti akinukuliwa na Marca.

"Nashukuru rais amezungumza na mimi kwa ukarimu sana na amenitaka nionyeshe mimi ni nani nikipata nafasi.

"Ni kweli kwamba ninapitia kwenye wakati mgumu sana kwa sasa, lakini ninaimani nitapata nafasi siku moja na kuonyesha uwezo wangu wa hali ya juu."

Umtiti alikuwa mmoja wa wachezaji ambao waliwekwa kwenye orodha ya kuuzwa msimu wa dirisha la usajili wa kipindi cha majira ya joto.

# Newcastle yaachana na kocha Bruce



**NEWCASTLE, London**

BAADA ya siku 13 tangu uongozi wa Newcastle uingie madarakani, wameamua kumtimua kocha wake, Steve Bruce.

Bruce anaondoka Newcastle United baada ya kuiongoza timu hiyo kwa muda wa miaka miwili.

Huu ni msimu ambao umekuwa mgumu na mbaya kwa 'The Magpies' hao, hadi sasa wakiwa hawajaonja ladha ya ushindi kwenye Ligi Kuu England ikiwa ni michezo nane.

Kuondoka kwa Bruce ni suala ambalo wengi walilitegemea akiwamo yeye mwenyewe.

Kabla ya Mike Ashley kuiuza timu hiyo, Bruce alinukuliwa akisema wazi kuwa, hana uhakika wa kuendelea kuwapo klabuni hapo endapo mabadiliko ya uongozi yatafanyika.

Nukuu ya Bruce, iliendelea kuwa hivyo hata baada ya wamiliki wapya kuingia madarakani na sasa yametimia.

Baadhi ya makocha wanahusishwa na nafasi ya kukinoa kikosi cha Newcastle ni Paulo Fonseca, Eddie Howe na Steven Gerrard.

Baada ya Bruce kuachana na timu hiyo, kocha huyu atapewa fidia ya takribani pauni milioni nane.

## HABARI MICHEZO

# 5,659,980 JACKPOT

## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/10/2021 | 17:00 | Leeds vs Wolverhampton | 2.33 | 3.41 | 3.01 |
| 02. 23/10/2021 | 17:00 | Millwall vs Stoke City | 2.37 | 3.16 | 2.97 |
| 03. 23/10/2021 | 17:00 | Peterborough vs QPR | 2.90 | 3.20 | 2.39 |
| 04. 23/10/2021 | 17:15 | Cadiz CF vs Alaves | 2.51 | 3.02 | 3.07 |
| 05. 23/10/2021 | 19:30 | Elche vs Espanyol | 2.71 | 3.02 | 2.82 |
| 06. 23/10/2021 | 22:00 | Athletic Bilbao vs Villarreal | 2.53 | 3.14 | 2.93 |
| 07. 24/10/2021 | 14:00 | Nice vs Lyon | 2.63 | 3.47 | 2.53 |
| 08. 24/10/2021 | 16:00 | West Ham vs Tottenham | 2.38 | 3.36 | 2.96 |
| 09. 24/10/2021 | 16:00 | Brentford vs Leicester | 2.62 | 3.27 | 2.72 |
| 10. 24/10/2021 | 17:15 | Barcelona vs Real Madrid | 2.65 | 3.54 | 2.53 |
| 11. 24/10/2021 | 18:30 | Stuttgart vs Union Berlin | 2.36 | 3.44 | 2.84 |
| 12. 24/10/2021 | 18:30 | Manchester Utd vs Liverpool | 3.07 | 3.62 | 2.21 |
| 13. 24/10/2021 | 19:00 | Roma vs Napoli | 2.62 | 3.43 | 2.62 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 22 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4347 | Urawa Red Diamonds vs Kashiwa Reysol | 1.82 | 3.33 | 4.05 |
| 16:00 | 1713 | Charlton U23 vs Millwall U23 | 2.30 | 3.55 | 2.90 |
| 16:00 | 4298 | Kagera Sugar vs Mtibwa Sugar | 1.97 | 3.00 | 4.50 |
| 17:00 | 1478 | Rio Ave U23 vs SP. Braga U23 | 3.28 | 3.48 | 1.99 |
| 18:30 | 1083 | Italy W vs Croatia W | 1.01 | 22.00 | 35.00 |
| 19:00 | 3323 | Dinamo Moscow vs FK Khimki | 1.47 | 4.24 | 6.31 |
| 19:30 | 1022 | Torino vs Genoa | 1.80 | 3.67 | 4.42 |
| 20:00 | 1427 | Yeni Malatyaspor vs Altay | 2.96 | 3.35 | 2.28 |
| 20:00 | 1685 | Annecy FC vs Cholet | 1.65 | 3.81 | 4.60 |
| 20:00 | 1887 | Boulogne vs Chateauroux | 2.79 | 3.08 | 2.49 |
| 20:00 | 2894 | Aston Villa U23 vs Sunderland U23 | 1.56 | 4.36 | 4.46 |
| 20:00 | 3178 | Eyupspor vs Adanaspor | 1.45 | 4.26 | 5.81 |
| 20:00 | 4230 | Orleans vs Avranches | 2.04 | 3.36 | 3.36 |
| 20:00 | 4418 | Switzerland W vs Romania W | 1.07 | 9.65 | 17.37 |
| 20:00 | 4626 | Ankaragucu vs Manisa BBSK | 1.94 | 3.39 | 3.53 |
| 20:00 | 5142 | Neman Grodno vs BATE Borisov | 4.37 | 3.59 | 1.70 |
| 21:00 | 1135 | Jong Utrecht vs FC Oss | 2.25 | 3.56 | 2.78 |
| 21:00 | 1904 | FC Eindhoven vs Jong Ajax | 2.17 | 3.86 | 2.74 |
| 21:00 | 2121 | Burnley U23 vs Middlesbrough U23 | 2.56 | 3.67 | 2.31 |
| 21:00 | 2615 | ADO Den Haag vs SBV Excelsior | 1.91 | 3.77 | 3.38 |
| 21:00 | 3233 | Derby County U23 vs Crystal Palace U23 | 2.62 | 3.59 | 2.30 |
| 21:00 | 3268 | NAC Breda vs Maastricht | 1.40 | 4.79 | 6.25 |
| 21:00 | 3425 | Almere City vs Jong PSV | 1.67 | 4.02 | 4.22 |
| 21:00 | 3732 | VVV Venlo vs De Graafschap | 3.71 | 3.76 | 1.82 |
| 21:00 | 4280 | Norwich U23 vs Birmingham U23 | 2.41 | 3.56 | 2.50 |
| 21:00 | 4447 | Dordrecht vs Den Bosch | 2.59 | 3.67 | 2.35 |
| 21:00 | 5079 | Arsenal U23 vs Everton U23 | 1.64 | 4.06 | 4.16 |
| 21:00 | 5170 | Leeds United U23 vs Brighton U23 | 1.89 | 3.97 | 3.19 |
| 21:00 | 5427 | Telstar vs Helmond Sport | 1.88 | 3.67 | 3.57 |
| 21:00 | 5509 | Willem II Tilburg vs Fortuna Sittard | 1.78 | 3.70 | 4.14 |
| 21:00 | 5516 | Jong AZ Alkmaar vs FC Volendam | 3.86 | 4.20 | 1.70 |
| 21:00 | 5746 | Fulham U23 vs Nottingham U23 | 2.08 | 3.57 | 3.00 |
| 21:15 | 3403 | Slovenia W vs Wales W | 2.09 | 3.73 | 2.86 |
| 21:30 | 2292 | FC Wil vs Neuchatel Xamax | 2.81 | 3.19 | 2.35 |
| 21:30 | 3143 | Alessandria vs Crotone | 2.81 | 3.30 | 2.40 |
| 21:30 | 3670 | FC Aarau vs FC Thun | 1.96 | 3.67 | 3.19 |
| 21:30 | 5956 | Mainz vs Augsburg | 1.71 | 3.68 | 4.78 |
| 21:35 | 4617 | Scotland W vs Hungary W | 1.21 | 6.20 | 9.30 |
| 21:45 | 1035 | UCD Dublin vs Treaty United | 1.63 | 4.05 | 4.25 |
| 21:45 | 1899 | Sampdoria vs Spezia | 1.69 | 4.11 | 4.51 |
| 21:45 | 2448 | Galway United vs Bray Wanderers | 2.19 | 3.34 | 2.95 |
| 21:45 | 3063 | Dungannon Swifts vs Carrick Rangers | 2.76 | 3.68 | 2.17 |
| 21:45 | 3595 | St Patricks vs Dundalk FC | 2.16 | 3.24 | 3.10 |
| 21:45 | 3892 | Bohemians FC vs Waterford Utd | 1.41 | 4.16 | 6.78 |
| 21:45 | 5505 | Iceland W vs Czech Republic W | 1.91 | 3.52 | 3.47 |
| 22:00 | 3368 | Arsenal vs Aston Villa | 1.98 | 3.54 | 3.74 |
| 22:00 | 4935 | St Etienne vs Angers | 2.54 | 3.19 | 2.79 |
| 22:00 | 5432 | Osasuna vs Granada | 1.82 | 3.52 | 4.52 |
| 22:00 | 5984 | Eibar vs FC Cartagena | 1.88 | 3.30 | 4.14 |
| 22:15 | 4331 | Vitoria Guimaraes vs Maritimo | 1.58 | 3.75 | 5.72 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# TUCHEL AFUNGUKA KUTETA NA HAALAND



**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, amesema klabu hiyo, imejadiliana kuhusu uhamisho wa Erling Haaland na hajaondoa uwezekano wa straika huyo wa Borussia Dortmund kuungana na Romelu Lukaku pale Stamford Bridge.

Haaland amekuwa akiwaniwa na klabu kadhaa, Ulaya baada ya kuwa na kiwango cha kuvutia kule Dortmund akifunga mabao 41 katika mechi 41 alizocheza, kwenye mashindano yote msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, amefunga mabao 70 katika mechi 69 kwa klabu hiyo ya Ujerumani tangu alipohamia hapo Januari 2020 - ni mshambuliaji wa Bayern Munich pekee, Robert Lewandowski (mabao 88 katika mechi 73), ambaye ana mabao mengi zaidi kushinda yeye.

Mkataba wake wa sasa amebakiza miaka miwili na nusu pale kwenye dimba la Signal Iduna Park na Dortmund hawana presha kumuuza straika wake huyo, baada ya kumtoa Jadon Sancho aliyetua Manchester United kwa pauni milioni 72.9.

Hata hivyo, kipengele cha kununuliwa kwa Euro milioni 75 kinafikia mwishoni mwa msimu huu na Tuchel ameonyesha ishara kuwa, Chelsea inaweza kukamilisha usajili wa straika huyo.

"Tulizungumza kuhusu Erling Haaland mara nyingi tu, ukiwamo wakati wa dirisha la uhamisho," alisema Tuchel akiiambia Sport Bild.

"Bado tunazungumza kuhusu yeye mara kwa mara, bilashaka kwa sababu yeye ni mchezaji muhimu na ni wazi kwamba tunamhitaji."

# Fati akubali mkataba mpya Barcelona



**BARCELOBA, Hispania**

ANSU Fati amekubali mkataba mpya wa muda mrefu pale Barcelona, ambao utamfanya kuwa hapo Camp Nou hadi mwaka 2027, klabu hiyo imetangaza.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania mkataba wake wa sasa ulikuwa unamalizika mwishoni mwa msimu huu, lakini Barca walikuwa na kipengele cha kumuongezea miaka miwili zaidi.

Fati amekuwa na mchango mkubwa tangu alipoanza kuichezea klabu hiyo Agosti 2019, na miamba hao wa Catalunya wameamua kumfunga ramsi klabuni hapo.

Tayari Pedri mwenye umri wa miaka 18, ameshajifunga Barca akiwekewa kipengele cha kuuzwa kwa Euro bilioni moja.

Fati amevunja rekodi kadhaa tangu alipotambulishwa mwaka 2019, ikiwamo kuwa mfungaji mwenye umri mdogo zaidi kuifungia Barca kwenye LaLiga akiwa na umri wa miaka 16 na siku 304.


Amerithishwa jezi namba 10 kutoka kwa Lionel Messi ambaye amehamia Paris Saint-Germain, pia ni mchezaji kijana zaidi kufunga kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mzaliwa huyo wa Guinea Bissau, amefunga mabao 15 katika mechi 48 za LaLiga hadi sasa.

# Michezo

Ijumaa Oktoba 22, 2021

Nipashe

## Ronaldo akunwa morali kikosini United

UKURASA 21

MTIFUANO...



Kocha Msaidizi wa Simba, Thierry Hitimana, akishuhudia mabeki wa timu hiyo, Mohamed Hussein 'Tshabalala na Henoc Inonga Baka 'Varane' (kulia), wakipambana mazoezini kujiandaa na mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana, itakayopigwa Jumapili katika Uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: SIMBA**

## Yanga yaipiga mkwara mzito Azam

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imeanza tambo kuelekea kwenye mechi ya raundi ya nne ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Azam FC itakayopigwa Oktoba 30, mwaka huu, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, baada ya kueleza kuwa itaingia na moto uleule ilioanza nao na kama kuna mtu wapinzani wao hao wanataka kumfukuza basi wafanye hivyo mapema ili wasionekane wao ndiyo chanzo.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, ndiye aliyetoa kauli hiyo jana, akifafanua kwamba wataingia kwenye mechi hiyo wakiiheshimu Azam, lakini hawaiogopi na watacheza kama walivyocheza mechi zingine za ligi, ingawa wanajua kuwa hukamiwa wanapocheza na wapinzani hao.

"Kuna watu wananiuliza eti mnaingia na tahadhari gani kwenye mechi yenu na Azam, hivi sisi Yanga ndiyo tuingie kwa tahadhari kweli? Mimi nadhani Azam ndiyo wanatakiwa kuingia kwa tahadhari kwenye mechi dhidi yetu. Wanatakiwa wawe na tahadhari la sivyo wanaweza kupigwa mabao mengi," alisema Bumbuli.

Alisema mechi dhidi ya Azam FC ni ngumu tu kama nyingine kwa sababu karibuni timu zote za Ligi Kuu huwa ni ngumu na zinapambana sana zikicheza na Yanga.

"Hata hao Azam, wakicheza dhidi ya Yanga ndiyo wanaachia silaha zao zote. Watapambana kwa kila hali na makocha wetu wanalijua hilo. Ila tunawaambia Azam wajiandae maana sisi hatuna uwanja mgumu, mwepesi, mzuri wala mbaya zitakuwa zinaguswa tu. Na kama kuna mtu anatakiwa kufukuzwa basi wafanye hivyo mapema ili isije kuonekana Yanga ndiyo sababu ya kufukuzwa kwake," alitamba Bumbuli.

Yanga mpaka sasa ndiyo vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa wameshinda mechi zote tatu, huku Azam ikikamata nafasi ya nane kwa pointi nne baada ya kupoteza moja, sare moja na kushinda moja.

# SIMBA SC YAITANGAZIA GALAXY 'IT'S NOT OVER'

## ●●● Yasema kazi iendelee kwa kuwashushia mafuriko Watswana hao Jumapili, Gomes afunguka...

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

KUELEKEA mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili wiki hii, uongozi wa Simba umekuja na kaulimbiu ya 'It's not Over'... Kazi Iendeleee, wakilenga ushindi wa kishindo kizito.

Katika mchezo wa awali uliopigwa Uwanja wa Taifa wa Botswana Jumapili iliyopita, Simba ilibuka na ushindi wa mabao 2-0, shukrani kwa Taddeo Lwanga na John Bocco walioizamisha Jwaneng Galaxy.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari Msaidizi wa Simba, Ally Shatry, alisema wamejipanga vizuri na kwamba licha ya kupata matokeo chanya nchini Botswana wiki iliyopita, lakini kazi bado haijaisha na wanahitaji kuendelea kupata matokeo katika mechi hiyo ya marudiano.

Alisema kikosi chao kimeingia kambini na kuendelea na maandalizi ya mchezo huo na wapinzani wao Jwaneng Galaxy tayari wamewasili nchini na kwa ajili ya mchezo huo.

"Maandalizi ya timu yanaendelea vizuri kwa kujiandaa na mchezo huo wa marudiano wa michuano hiyo, dhidi ya Jwaneng Galaxy licha ya kupata ushindi ugenini, lakini bado kazi inaendelea kuhakikisha tunapata ushindi na kuingia makundi," alisema Shatry.

Simba tayari wameanza kuuza tiketi za mechi hiyo, ambazo zinapatikana kupitia mitandao yote ya simu kwa Sh. 7000 kwa mzunguko huku VIP B na C ikiwa ni Sh. 20,000, VIP A Sh. 40,000 wakati Platinum ikiwa ni Sh. 150,000.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, alisema ana imani kubwa na wachezaji wake kupata matokeo mazuri katika machezo huo wa marudiano na anahitaji kuona washambuliaji wake wakiwa makini kuhakikisha katika kuzifumania nyavu.

Alisema mechi ya kwanza hali ya hewa ilikuwa shida kwao, lakini ana imani mchezo huo wa marudiano wanaocheza nyumbani watakuwa vizuri na kupambana kupata ushindi mkubwa kuwani watakuwa katika hali ambayo wameizoea.

"Tunahitaji kupata matokeo mazuri ya ushindi mkubwa kwa kuhakikisha tunatumia vizuri nafasi tunazozipata ili kushinda kwa idadi kubwa ya mabao, licha ya kuhitaji ushindi, sare aina yoyote au sare ili tuingie rasmi hatua ya makundi," alisema Gomes.

Alisema maandalizi yanaendelea vizuri na wamejipanga kuhakikisha wanafanya vizuri zaidi katika mchezo huo ambao kama Galaxy hawatapindua meza basi Simba itatinga hatua ya makundi ikiwa ni kwa msimu wa pili mfululizo kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika, CAF.

Gomes alisema wachezaji wake wote wako fiti isipokuwa mshambuliaji Chris Mugalu na kiungo Pape Sakho, ambao ataendelea kuwakosa kutokana na kuwa nje ya dimba wakiuguza majeraha.

Naye Meneja wa klabu hiyo, Patrick Rweyemamu, alisema wanaupa umuhimu mkubwa mchezo huo ambao anaamini kama wakiendelea kufanya vizuri uchumi wa klabu yao utazidi kukua kupitia michuano hiyo ikiwa ni pamoja na kulitangaza zaidi soka la Tanzania kimataifa.

Alisema wachezaji wote wapo vizuri kisaikolojia kuelekea mechi hiyo na kila mmoja ana kiu ya kucheza ili kuendeleza ushindani kama walivyofanya katika mchezo uliopita.

"Wachezaji wameahidi kuendeleza ushindani katika mchezo huo ambapo watakuwa kwenye uwanja wetu wa nyumbani tunaomba Watanzania wazidishe dua zao," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >